tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Hatari** za kiafya waendesha boda,nguo za kubana

UKURASA 3




UKURASA 9

Jumapili Agosti 27, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581415

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Madereva daladala katika balaa kubwa

• **Madaktari,** polisi waanika mambo yanayoshtua.. *Ukurasa 2*



Baadhi ya madereva wa daladala wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### SERIKALI YATAFITI SABABU UFAULU KIDUCHU HISABATI

SERIKALI kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imefadhili miradi ya kimkakati ikiwamo wa kutafiti wanafunzi kutofanya vizuri...



## Muhimbili yafanya upasuaji bandama kwa mara ya kwanza

UKURASA 2

## Serikali yaingilia kati uhaba Dola, mafuta

UK. 3

MICHEZO YANGA USO KWA USO NA AL MERREIKH UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Mwenyekiti wa kikundi cha Wanawake cha Mwangaza, Gaudensia Mgedela, akikabidhi zawadi kwa mwakilishi wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa Shule ya Sekondari Pugu, wakati wa Maadhimisho ya Miaka 10 tangu kuanzishwa kwa kikundi hicho, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

## Muhimbili yafanya upasuaji wa kwanza bandama

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imefanya upasuaji mkubwa wa kuondoa bandama lenye shida kwa mgonjwa kwa njia ya matundu madogo (laparoscopic splenectomy).

Upasuaji huu ni wa kwanza kufanyika hapa nchini ambao umefanywa na madaktari wa upasuaji wa MNH kutokana na ubobezi walionao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma (MNH), Aminiel Aligaesha, upasuaji huo umeongozwa na Dk. Kitembo Kibwana, mbobezi wa upasuaji mfumo wa chakula na ini.

Alisema mbobezi huyo ndiye aliyeongoza jopo la madaktari, wauguzi na watalaamu wa ganzi na usingizi kufanya upasuaji huo.

"Bandama (wengu) ni kiungo cha mwili chenye nafasi katika mzunguko wa damu. Lipo ndani ya fumbatio ya mwili karibu na mfuko wa chakula ambapo kazi yake kubwa ni kuongeza seli nyeupe za damu na kuondoa seli nyekundu za damu zilizozeeka.

"Kwa watoto ina jukumu la kutengeneza seli nyekundu za damu. Watu wazima kwa kawaida wanaweza kuishi bila ya bandama," alisema.

Alisema Hospitali ya Muhimbili inaendelea kuboresha huduma zake mbalimbali ikiwamo upasuaji mkubwa, uchunguzi na mifumo ya utoaji huduma kwa ujumla wake.

# Madereva daladala katika balaa zito

**Na Waandishi Wetu**

JARIBU kufikiria kuhusu maisha ya madereva wa mabasi madogo ya abiria, maarufu kama daladala, katika miji mikubwa nchini. Wengi wao wanaamka saa 10 alfajiri na kulala usiku wa manane.

Mbali na kutolala kwa muda mrefu, madereva hao wanaitaja kazi hiyo kuwa na vikwazo vingi barabarani, vikiwamo foleni wakati wakitafuta 'hesabu' za wamiliki wa vyombo hivyo.

Kwa nyakati tofauti katika mazungumzo na Nipashe Jumapili, baadhi ya madereva hao mkoani Dar es Saalam, wamekitaja kikwazo kikubwa zaidi kwao ni kukamatwa mara kwa mara na askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, maarufu kama Trafiki, na kupigwa faini kutokana na makosa mbalimbali ya barabarani.

Dereva Ally Hassan anayeendesha daladala kwa safari kati ya Segerea na Kawe, anasema: "Kazi hii ina changamoto nyingi. Kila siku ninaamka saa 10 alfajiri na kulala kati ya saa 6:00 au 7:00 usiku. Jambo hili hunisababishia kukosa usingizi hata ninapotaka kupumzika.

"Changamoto nyingine ya kiafya ninayokutana nayo ni kushindwa kuona vizuri. Tunapata matatizo ya macho kutokana na vumbi na wakati mwingine kuugua magonjwa mara kwa mara, hasa ya mfumo wa hewa. Kumbuka katika daladala wanapanda watu wa aina tofauti. Sisi tuko katika hatari ya kupata magonjwa ya kuambukiza muda wowote."

Dereva Hassan anataja changamoto nyingine kazini ni kuumwa nyonga na mgongo kutokana na kutumia muda mwingi kukaa na kushikilia usukani.

Dereva mwingine, Said Juma, anawanyooshea kidole trafiki kwamba wamekuwa sehemu ya vikwazo kwa utendaji wa madereva wa daladala kutokana na ukamataji holela.

"Nipo kwenye kazi hii kwa miaka mitano sasa, lakini kutokana na kamatakamata za mara kwa mara, kwangu hii ni changamoto kubwa. Wakati wote nikiwa barabarani ninajikuta ninafanya kazi kwa kutojiamini. Nikiona tu trafiki, hata kama sina kosa, ninawaza kukamatwa au kupigwa faini," anasema.

Naftali Kimaro, dereva wa daladala inayofanya safari za Makumbusho hadi Simu 2000, anasema amekuwa akiamka saa 11:00 alfajiri kila siku na kushikilia usukani hadi saa 5:00 usiku, inapotokea kutopata hesabu ya bosi ambayo ni Sh. 90,000 kwa siku, hulazimika kuongeza saa mbili zaidi za kuendelea na kazi hadi usiku wa manane.

Anasema kazi yao hiyo pia ina kikwazo kingine, baadhi yao hawana mikataba ya kazi, hivyo kukosa stahiki mbalimbali za kiutumishi. Ni dosari anayoitaja inawafanya kuendelea kuishi maisha magumu na wakati mwingine kushindwa kuendesha familia.

Changamoto zingine. Kimaro anazitaja kuwa ni kukosa muda wa kupumzika, kutokuwa na bima ya afya jambo ambalo kwao ni tatizo kubwa kwa kuwa wanapougua wakati mwingine hushindwa kujihudumia na kufikia hatua ya kuomba misaada kwa wengine.

Kimaro alitaja changamoto nyingine ni askari polisi wanaofanya operesheni zao usiku. Wamekuwa wakiwakamata na wakati mwingine wakiwa hawana makosa na kuwataka watoe fedha ili kuwaachia.

"Ninaomba mamlaka husika isaidie kutatua kero hii kwa sababu wakati mwingine gari la polisi limeandikwa RTO (mkuu wa usalama barabarani) la Kinondoni, limekuwa likifukuzana na daladala na endapo dereva hatakuwa makini, kunaweza kusababishwa ajali," anasema.

Dereva wa daladala inayofanya safari za Mawasiliano-Masaki, Omari Omari, anasema: "Changamoto kubwa ni kukosa muda wa kupumzika na wakati mwingine unajikuta upo barabarani huku unasinzia."

Omari alitaja changamoto nyingine kuwa ni vumbi ambalo limekuwa likisababisha matatizo ya macho na kuathiri utendaji wao barabarani.

"Foleni kubwa wakati mwingine ni kero kwetu, inachangia kwa kiasi kikubwa mwisho wa siku tunashindwa kufikisha hesabu za bosi," anasema Dereva Mohamed Pengo anayefanya safari za Mabibo-Gerezani.

Anaitaja changamoto ya foleni imekuwa inasababisha waingie katika mgogoro na trafiki kwa sababu hulazimika kuvunja sheria na kutanua na inaposhindikana hukaa muda mrefu eneo moja na kushindwa kutimiza hesabu ya siku.

**MULIRO AFUNGUKA**

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna msaidizi Mwandamizi Jumanne Muliro, alipotafutwa na Nipashe Jumapili kuzungumzia changamoto zinazodaiwa kulikumba kundi hilo, alisema daladala zinazokamatwa ni zile zenye makosa na madeni na si kwa sababu ya kufanya biashara usiku.

"Kuna magari ambayo ni mabovu na kuna mengine yana makosa na yameandikiwa faini. Kwahiyo, wanachofanya wanayapaki mchana, wanakuwa wanasubiri usiku ndipo wayatoe wakiamini kwamba askari polisi wamelala.

"Na wengi kwa sababu hiyo, huanza kutoa magari kuanzia saa nne usiku. Wasisingizie kwamba wanakamatwa kwa sababu ya kufanya kazi usiku, huo ni uongo. Wanakamatwa kwa sababu ya madeni yao. Na hata ukienda gereji utakuta magari yamepaki, ila usiku wanayatoa," alisema.

Kamanda Muliro alisema oparesheni hiyo si kwa Kinondoni pekee, bali kwa mikoa yote ya Kipolisi Dar es Salaam.

**MTAALAMU AFYA**

Katibu Mkuu wa Chama cha Madaktari wa Michezo Tanzania, Dk. Sufian Juma, anasema dereva anapokaa kwa muda mrefu kwenye gari, anajiweka katika hatari ya kupata tatizo kwenye uti wa mgongo.

"Mtu anaposimama, uzito wake unategemea vifundo vya mguu pamoja na magoti, na anapokaa uzito wake unategemea uti wa mgongo na kiuno. Kwa hiyo, anapokaa muda mrefu anajitengenezea matatizo ya mgongo," anafafanua.

Dk. Sufian anawashauri madereva wawe na tabia ya kutenga muda wa kupumzika ili kujiepusha na matatizo hayo.

"Tiba zipo, mtu anaweza kutibiwa mpaka akapona kabisa, lakini kinga ni bora kuliko tiba. Ni vyema mtu achukue tahadhari ya afya mapema," anashauri.

* **Imeandaliwa na Elizabeth Zaya, Khalfan Chusi, Neema Msalaba (UDSM), Ester Mbilinyi na Khadija Kategile ((TUDARCo)**

## HABARI KITAIFA

# Hatari kiafya waendesha bodaboba, wanaovaa nguo zenye kubana mwili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Mkojo na Uzazi wa wanaume katika Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa, Remigius Rugakingira, amesema waendesha bodaboda wanaobeba abiria kwa mtindo wa mishikaki na kukalia tangi la mafuta, wako hatarini kupoteza nguvu za kiume.

Mtaalam huyo analitaja kundi lingine lililo hatarini ni vijana wanaovaa nguo za kubana (skin jeans), na boxer zinazobana korodani kuwa nao hawako salama ikiwa wataendelea na tabia hizo kwa muda mrefu.

Dk. Rugakingira aliyasema hayo jana jijini Dodoma akieleza kuwa madereva hao wako hatarini kukabiliwa na upungufu wa nguvu za kiume siku za usoni kwa sababu ya kukalia matangi hayo ambayo hupata joto baada ya pikipiki kutembea mwendo mrefu.

"Kwanza mafuta yenyewe ni kemikali. Tangi linaloyahifadhi hupata joto pikipiki ikitembea kwa muda mrefu, hivyo kwa mwendeshaji kukaa juu yake maana yake hupokea joto hilo kwenye korodani ambayo ni kiwanda cha kuzalisha mbegu za uzazi na vichocheo vinavyochangia uume kusimama," alisema Dk. Rugakingira

Kwa mujibu wa daktari huyo, korodani huhimili joto la kiwango kinachotakiwa akitolea mfano kuwa kunapokuwa na baridi kali huingia tumboni kuepuka baridi, vivyo hivyo joto linapozidi huziweka hatarini.

"Ingawa tafiti za kisayansi zinaonesha kuwapo kwa visababishi mbalimbali vya maradhi ya upungufu wa nguvu za kiume kama mtindo wa maisha hasa ulaji usiyofaa.

"Kutoshughulisha miili na saikolojia ya washiriki wa tendo la ndoa, upo ushahidi wa kisayansi kuwa wanaume wanaofanya kazi katika mazingira ya joto huathiriwa na tatizo hilo," alisema.

Dk. Rugakingira aliwataka vijana kuwa makini na maelekezo wanayopewa na wataalam wa afya ili kuepuka kupata magonjwa ambayo yanatokana na kupanda mshikaki.

Alisema vijana wote wanaofanya vitendo hivyo, wanapaswa kubadilika mapema ili kuepuka kupata matatizo mbalimbali ya kiafya.

Kwa upande Julius John, alisema ni vyema elimu kuhusu hilo iendelee kutolewa kwa madereva ili waweze kutambua madhara ya kupanda mishikaki.

"Ninaiomba serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii hususani madereva bodaboda ambao wanapenda kupakiza abiria kwa mtindo wa mishikaki,"alisema John.

Alisema ni vyema kila dereva bodaboda akalijua hilo ili aweze kujiepusha na mawazo ya upakiaji huo badala yake, wafuate sheria za uendeshaji bodaboda.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya TOL GASES, Daniel Warungu (katikati) akizungumza katika Mkutano Mkuu wa 28 wa wanahisa wa Kampuni hiyo Dar es Salaam jana.Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni hiyo, Saimon Mponji na Katibu wa Kampuni hiyo, Cornelius Kariwa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Serikali yaingilia kati uhaba wa Dola

**Na Halfan Chusi**

SERIKALI imesema katika kukabiliana na uhaba wa Dola wenye athari kiuchumi, imewarejeshea wafanyabiashara wa maduka ya kubadilishia fedha Sh. bilioni tisa, huku ikifanya tathmini kama kuna haja ya kuweka ruzuku kwenye mafuta.

Imesema mpaka sasa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeuza Dola za Marekani milioni 20 kwa benki na hatua nyingine mbalimbali zinaendelea ,zikiwamo kutekeleza sera ya BoT kununua dhahabu ambapo katika kipindi cha Mei hadi Julai, mwaka huu, imenunua zaidi ya kilo 4,000.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, alitaja hatua zingine ambazo serikali imechukua kuhusu uhaba wa Dola kuwa ni kuongeza utafutaji wa mikopo, serikali kuwawezesha wafanyabiashara kwa kuwapatia shilingi ili wapate Dola.

Pia alisema kutoa dhamana ya bidhaa zinazouzwa nje na kuunga mkono wafanyabiashara na wawekezaji kuongeza mauzo ya ndani ya nchi. Kadhalika, alisema hatua nyingine ni kutoa leseni kwa maduka ya kubadilishia fedha ambapo mpaka sasa zilizotolewa zimefikia 80.

"Wale walionyang'anywa leseni zao baadhi wamesharejeshewa. Wale ambao hawajakidhi vigezo wanashughulikia, walionyang'anywa fedha mpaka sasa Sh. bilioni tisa zimesharejeshwa kwao ili waendelee na biashara," alisema.

Msigwa alisema hatua zingine serikali inazochukua ni kuhimiza kuongeza uzalishaji kwa bidhaa za kilimo, madini na mifugo kuuzwa nje ili kuongeza Dola nchini.

Kuhusu ruzuku katika mafuta, Msigwa alisema serikali inaendelea kufanya tathmini ili kuona kama inaweza kufanya hivyo.

"Tunatathmini tuone. Tuache huduma zingine tuweke huku, ikilazimu kufikia hatua hiyo, tutafanya. Wachumi na wataalam wetu wanaangalia tufanye kipi, tutoe wapi? Tuweke wapi? Ili angalau tusikose, unaweza kuleta furaha kwenye bei ya mafuta alafu watanzania wakakosa dawa, watakufa siyo," alisema.

Kuhusu suala la uendelezaji wa bandari, Msigwa alisema serikali inaendelea kupokea maoni na kwamba yatazingatiwa wakati wa kufunga mikataba ya utekelezaji wa mradi.

Akizungumzia majaribio ya mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambayo serikali iliahidi kufanyika Julai, mwaka huu, alisema suala hilo lilishindikana kwa sababu baadhi ya vipuri ambavyo ni muhimu vilichelewa kufika.

Hata hivyo, alisema wakati wowote watatoa taarifa ya lini jaribio hilo litafanyika.

Kuhusu maendeleo ya mradi huo kwa ujumla alisema: "Hadi kufikia Julai, mwaka huu, kipande cha kwanza cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) kimefikia asilimia 99 huku ujenzi wa njia kuu ya reli, mifumo ya ishara na mawasiliano na miundombinu ya umeme ikiwa imeshakamilika.

"Kazi zinazoendelea katika kipande hiki ni majaribio ya mifumo mbalimbali ya uendeshaji katika stesheni na njia kuu ya reli pamoja na kazi za ujenzi wa vivuko vya juu inayoendelea vizuri katika maeneo ya Vingunguti, Airport na Banana/majumba sita jijini Dar es Salaam."

Msigwa alisema katika kipande hiki ujenzi wa njia ya reli kuingia Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya treni za mizigo unaendelea.

"Kipande cha pili Morogoro - Makutupora (km 422) kimefikia asilimia 94.74 na ujenzi wa vivuko vya barabara unaendelea vizuri ukiwa katika hatua za mwisho.

"Ujenzi wa stesheni zote umekwishakamilika isipokuwa kwa stesheni ya Dodoma ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 73.29 na kazi za umaliziaji zinaendelea. Kipande hiki pia kinahusisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya TRC jijini Dodoma ambalo limefikia asilimia 97.59," alisema.

Msigwa alisema kazi za ujenzi wa uzio katika njia ya reli zimefikia asilimia 78.41, ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme umefikia asilimia 98.65 na ufungaji wa mifumo ya ishara na mawasiliano ya reli umekamilika kwa asilimia 89.74.

"Katika kipande hiki cha pili, ujenzi wa kituo cha mizigo na karakana ya treni za kisasa pia unaendelea katika eneo la Ihumwa jijini Dodoma ambapo tayari majengo ya kituo hicho yameshakamilika na kazi za ujenzi wa mifumo ya maji taka zinaendelea," alisema.

Kipande cha tatu cha Makutupora - Tabora (km 368), alisema kimefikia asilimia 10.06 na mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi.

"Kipande cha nne cha kutoka Tabora hadi Isaka (km 165) kimefikia asilimia 4.10, mkandarasi anaendelea na ujenzi wa kambi za ujenzi katika maeneo ya Bukene na Nzubuka. Kipande cha tano, cha kutoka Mwanza - Isaka (KM 341) ujenzi umefikia asilimia 37.22, kazi za ujenzi wa tuta la reli umefikia asilimia 73.5," alisema.

Msigwa alisema katika awamu ya pili ya ujenzi wa SGR kipande cha kutoka Tabora - Kigoma (KM 506) mkandarasi tayari yuko eneo la ujenzi akiendelea na kazi za awali za maandalizi ikiwamo ukusanyaji wa vifaa na ujenzi wa kambi za ujenzi.

"Mchakato wa utwaaji wa ardhi na ulipaji fidia kwa ajili ya ujenzi wa kambi zote tatu za ujenzi (Urambo, Nguruka na Uvinza) umekamilika," alisema.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 96/2023**
**MDAI: KESANTA THOBIAS**
**DHIDI YA**
**MDAIWA SALEHE RAJABU**
**KWA: SALEHE RAJABU wa TUNGI MOROGORO**

**OMBI LA MDAI:**
Anamtafuta mdaiwa ili aweze kuhudhuria Mahakamani kusikiliza madai yake yanayo mkabili.

**Madai ya:** Madai ya Fedha Tshs. 1800,000/= pamoja na gharama za shauri

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika Shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 29 Mwezi 08 Mwaka 2023 Saa 3:00 Asubuhi.

**Angalia kama** hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo terehe 23/08/2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

# Waziri ataja vipaumbele ardhi kwa ma-RC, ma-RAS

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maedeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewasilisha vipaumbele vya wizara kwa wakuu wa mikoa na makatibu tawala katika semina ya uongozi katika Chuo cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani.

Katika wasilisho lake jana, Waziri Mabula alizungumzia masuala ya ukusanyaji mapato yatokanayo na sekta ya ardhi, mipango miji na maeneo ya uwekezaji ambayo yote wakuu hao wa mikoa wanalo jukumu la kusimamia kwenye mikoa yao.

Dk. Mabula aliwataka wakuu wa mikoa kusaidia katika kuongeza hamasa katika suala la ukusanyaji mapato ya serikali yatokanayo na sekta ya ardhi.

"Niwaombe mkasimamie mikakati ya ukusanyaji maduhuli hayo ikiwa ni pamoja na kuwakumbusha wananchi waliopo katika maeneo kulipa kodi ya pango la ardhi, alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa msamaha wa riba ya kodi kwa miezi 10 na mafanikio yalionekana japo si kwa kiwango kilichotarajiwa.

Pia aliwataka wakuu wa mikoa kuzisimamia halmashauri katika kutenga fedha katika bajeti za maendeleo ya sekta ya ardhi ili kuhakikisha ardhi inapangwa, kupimwa na kumilikishwa.

"Halmashauri zitambue kuwa jukumu hilo bado ni la kwao na wanahitaji kuendelea kushiriki kikamilifu katika kutenga fedha ili kutekeleza majukumu yao na kuwezesha watumishi waliopo katika halmashauri kufanya kazi" alisema Dk. Mabula.

# Serikali yatafiti sababu ufaulu kiduchu Hisabati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imefadhili miradi ya kimkakati ikiwamo wa kutafiti wanafunzi kutofanya vizuri kwenye somo la Hisabati ili kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Amos Nungu, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2022/23 na mwelekeo wa vipaumbele vya taasisi kwa mwaka 2023/24.

Alisema kila matokeo yanapotoka ya darasa la Saba na Kidato cha Nne somo hilo limeonekana kuwa tatizo.

"Katika kufanya utafiti huo wa somo la hisabati serikali kupitia COSTECH imefadhili miradi miwili ambayo kila mmoja una thamani ya Sh. milioni 120 na utekelezaji wake unahusisha watafiti kutoka vyuo mbalimbali nchini na itafanyika ndani ya miaka miwili, sasa ipo hatua ya kusaini mikataba,"alisema.

Alisema kuwa utafiti huo utaangalia tatizo na njia ya kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

Kuhusu mapinduzi ya nne ya viwanda, Dk. Nungu alisema tume hiyo imeidhinisha miradi saba yenye thamani ya Sh. milioni 150 kila mmoja itakayofanyika ndani ya miaka miwili na inahusisha watafiti na wabunifu kutoka sekta zote za umma na binafsi.

"Mapinduzi ya nne ya viwanda yanahusu uelewa wa kutosha na matumizi ya teknolojia mbalimbali. Katika kuratibu Utafiti na Ubunifu, COSTECH tunaendelea kufanya kazi na wadau mbalimbali, kubwa ni kufanikisha kuweka mazingira wezeshi na upatikanaji wa rasilimali fedha,"alisema.

Akizungumzia vipaumbele vya tume kwa mwaka wa fedha 2023/24, alisema wamejipanga kushirikiana na mabaraza ya kikanda na kimataifa kuhakikisha wanashiriki kutafuta fursa ambazo zitaendelea kuleta fedha za utafiti kupitia COSTECH au kuhamasisha taasisi za ndani kuomba hizo fursa.

"Pia kupitia mradi wa HEET, tunaboresha mifumo mbalimbali ili kuongeza ufanisi zaidi katika suala la uratibu wetu, ikumbukwe kuwa mradi huu ni mahususi kwa Taasisi za Elimu ya Juu, sasa inabidi tuwe tayari kuwahudumia baada ya kukamilisha mabadiliko wanayofanya kupitia mradi huu wa HEET," alisema.

Alisema pia kufanya kazi na kumbi za bunifu na wadau wengine kuhakikisha mazingira wezeshi yanaimarika zaidi. Alisisitiza kuwa utafiti ni muhimu kwa dunia ya leo ili kuboresha au kuleta ufanisi katika maisha.



Mteja (kulia), akichagua kitoweo cha nyama ya kuku katika eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# TANROADS yawatoa hofu wananchi kuhusu ubora vifaa vya ujenzi miradi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Barabara (TANROADS) umewatoa hofu Watanzania kuhusu ubora wa vifaa vinavyotumika katika utekelezaji wa miradi inayoendelea kuwa ni imara na bora.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Mohamed Besta, alitoa ufafanuzi huo jana mkoani Dodoma baada ya kufanya ziara ya ukaguzi katika maabara inayotumika kupima viwango na ubora wa vifaa.

Pia alifanya ukaguzi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma sehemu ya pili kutoka Nala-Veyula-Mtumba (kilometa 52.3) ambayo hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 51.

Wakati wa ukaguzi huo, Mhandisi Besta aliwataka wataalamu hao kuhakikisha vifaa vyote vya ujenzi zikiwamo nondo, kokoto, udongo vinapimwa kwa weledi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa katika utekelezaji wa miradi.

"Serikali inatumia fedha nyingi katika utekelezaji wa miradi yake, hivyo wataalamu ambao mmeaminiwa kusimamia miradi hii pamoja na mshauri mwelekezi hakikisheni mnapima malighafi zote za ujenzi. Endapo mtakuta hazikidhi vigezo visitumike katika mradi wowote," alisema Besta.

Alisema katika kuhakikisha ubora na viwango vya ujenzi vinazingatiwa, wanaendelea kufuatilia upimaji wa malighafi zote zinazotumika katika miradi yote inayosimamiwa na TANROADS ili kuhakikisha barabara na madaraja yanayojengwa yanadumu na kukidhi thamani ya fedha.

"Miradi yote iliyoko chini ya TANROADS inafuatiliwa kwa umakini na ubora kulingana na thamani ya fedha ambayo imewekwa" alisema.

Mhandisi wa vifaa, anayesimamia mradi wa barabara ya mzunguko wa nje jijini Dodoma, Deogratius Nyambo, alisema vifaa vyote kabla havijaanza kutumika huingizwa katika maabara kwa ajili ya kupimwa ubora na endapo vitabainika havijakidhi huondolewa sehemu ya mradi.

Alisema katika kusimamia ubora kuna kazi za kila siku zinazofanyika ikiwamo kupima ubora wa udongo, tabaka la tuta la barabara kulingana na viwango vilivyowekwa vya mradi husika ili kuhakikisha barabara na madaraja zinadumu kwa muda mrefu.

Barabara ya mzunguko wa nje wa Jiji la Dodoma (kilomita 112.3) ambayo ujenzi wake umegawanywa katika sehemu mbili, ambazo ni Nala-Veyula-Mtumba (Km 52.3) na Ihumwa-Matumbulu-Nala (Km 60) unatarajiwa kukamilika Desemba, mwakani.

Barabara hiyo pamoja na mambo mengine, itapunguza msongamano katika jijini la Dodoma na kuchochea shughuli za kiuchumi.

## HABARI KITAIFA

# UVCCM kuwapa mbinu vijana kuona fursa

**Na Restuta James**

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umewashauri vijana kujitokeza kwa wingi kwenye semina za kuwajengea uwezo, ili wapate mbinu za kuona fursa na kujiingizia kipato.

Katibu wa Idara ya Uhamasishaji na Chipukizi wa UVCCM Taifa, Edna Lameck, alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ziara ya Mwenyekiti wa UVCCM, Mohamed Ali Kawaida, kwenye mikoa mbalimbali.

Alisema vijana wengi wanajihusisha na ujasiriamali na wanategemea mikopo, hivyo UVCCM itaendelea kuwajengea uwezo wajikite kwenye malengo ya kujipatia maendeleo.

"UVCCM imekabidhiwa jukumu la kuwasemea vijana wote Tanzania wenye vyama na wasio na vyama. Tunaendelea na ziara nchi nzima ili kukutana na makundi mbalimbali ya vijana ambao wanajihusisha na shughuli za kimaendeleo," alisema.

Lameck alisema umoja huo pia unaibua mbinu na njia ambazo zitawasaidia vijana kujikwamua kiuchumi na kuijenga nchi yao.

"Tumeona namna ambavyo serikali inavyowawezesha kupitia mikopo ya asilimia 10 kwenye Halmashauri zetu, vijana wamehamasika na wamejikita kwenye ujasiriamali," alisema.

Katibu huyo aliwaalika vijana na wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kuhudhuria mkutano wake ambao utafanyika leo katika viwanja vya Zakhem, Mbagala ambao utahutubiwa na Kawaida pamoja viongozi waandamizi wa UVCCM Taifa.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Prof. Mark Mwandosya (wa pili kulia), akisikiliza maelezo ya hatua iliyofikiwa ya utengenezaji wa matela maalum kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Superdoll, Seif Seif, wakati bodi hiyo ilipotembelea karakana inayotengeza matela hayo yatakayotumika kusafirisha mabomba ya mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).
**PICHA: DENNIS FUSSI**

# Serikali kuyaenzi mazuri ya Membe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kuyaenzi mambo yote mazuri yaliyofanywa na marehemu, Bernad Membe wakati wa utumishi wake serikalini.

Marehemu Membe ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alifariki dunia Mei 12, mwaka huu, katika Hospitali ya Kairuki, Dar es Salaam, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Majaliwa aliyasema hayo jana aliposhiriki ibada ya kumbukumbu ya marehemu Membe iliyofanyika nyumbani kwao, Rondo, mkoani Lindi.

Alisema Membe enzi za uhai wake alikuwa mwanadiplomasia mahiri kwenye medani za kitaifa na kimataifa, hivyo serikali na Watanzania wataendelea kumkumbuka.

Alisema weledi, nidhamu, uchapakazi na umahiri wa marehemu Membe uliitambulisha Tanzania katika medani za kimataifa na kutengeneza marafiki na mataifa mengine.

"Mheshimiwa Membe alikuwa na weledi wa kitaifa na kimataifa, jumuiya za kimataifa zinatambua umahiri wake na alijizolea sifa kwa sababu ya nidhamu na uchapakazi wake," alisema.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akizungumza kwa niaba ya familia ya marehemu, aliishukuru serikali kwa ushirikiano ilioutoa katika kipindi cha msiba.

"Namshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa kanisa ulioanzishwa na marehemu Membe, " alisema.

# EWURA yaridhishwa utengenezaji wa matela ya kusafirishia mabomba

**Na Dennis Fussi**

BODI ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeeleza kuridhishwa na utengenezaji wa matela maalum 300 unaofanywa na kampuni ya Superdoll kwa ajili ya kusafirisha mabomba ya mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) pindi yatakapowasili nchini.

EWURA ndiyo ilitoa kibali cha mradi huo kwa upande wa Tanzania litakaloanzia Hoima nchini Uganda hadi Pwani ya Chongoleani mkoani Tanga, likiwa na urefu wa kilometa 1,443 na kati ya hizo, kilometa 1,147 ziko upande wa Tanzania. Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya, alisema katika ziara ya kutembelea karakana ya Superdoll iliyoko barabara ya Nyerere, Dar es Salaam, mjumbe wa bodi hiyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati, Haruna Masebu, alisema wameridhishwa na kazi ya utengenezaji wa matela hayo maalum yenye urefu wa mita 18.

Masebu alisema kati ya matela 300, matela 217 tayari yameshatengenezwa na mengine yaliyobaki yako katika hatua nzuri za umaliziaji.

"Haya matela yanatengenezwa kwa kibali maalum kwa ajili ya kazi ya usafirishaji wa mabomba kwenda kwenye maeneo husika yatakayopita mkuza. Tukiwa wadau muhimu wa serikali katika kusimamia utekelezaji wa mradi huu, tumeridhishwa na kazi na viwango vya matela haya yenye vifaa maalum kwa ajili ya usalama wa barabarani," alisema. Naye Meneja wa Petroli kutoka EWURA, Gevald Maganga, alisema waliamua kutembelea karakana hiyo ya Superdoll ili kuona maendeleo ya kazi hiyo, ambayo kwa kiasi kikubwa imefanyika kwa ufanisi na kuzingatia viwango vya kimataifa, kama mradi wa EACOP unavyotaka.

Naye MkurugenziMtendaji wa Superdoll, Fulgence Bube, alisema magari hayo yameombewa kibali maalum na wameshirikisha idara mbalimbali za serikali ikiwamo Wakala wa Barabara (TANROADS) ili kuhakikisha yanakidhi vigezo vya kupita katika barabarara bila kufanya uharibifu na kuzingatia usalama wa watuamiaji wengine.

Katika kuhakikisha msafara wa magari hayo hausababishi foleni, Bube alisema wataruhusu magari 20 tu kwa siku ili kuondoa usumbufu kwa sababu ya urefu wake.

"Haya matela yana urefu wa mita 18, ukijumlisha na kichwa yanaweza kufikia hadi mita 20, hivyo ni marefu sana ukilinganisha na malori yenye urefu wa kawaida wa mita 12," alisema.

Meneja Rasilimali Watu wa kampuni ya East African Logistics Services (EALS) Limited, inayoshirikiana na Superdoll katika kazi hiyo kupitia kampuni yake ya Superstar, Busegi Kulwa, alisema matarajio ni kumaliza matela yaliyobaki ndani ya kipindi kifupi ili kazi hiyo ianze mara moja.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera serikali kusikia kilio waagizaji wa mafuta

**WIKI** hii Chama cha Waagizaji wa Mafuta Tanzania (TAOMAC) kilipaza sauti kuhusu wanachama wake kushindwa kupata mafuta waliyoagiza kutoka nje ambayo yako katika matangi ya kuhifadhia nishati hiyo kutokana na kukosekana kwa Dola ya Marekani, sarafu ambayo inatumika kwa ajili ya miamala ya biashara hiyo.

Katika taarifa ya chama hicho, kumekuwa na uhaba wa mafuta katika vituo vingi kwa sababu ya kutokupatikana kwa bidhaa hiyo hatua ambayo inawafanya watumiaji wa nishati hiyo kupata adha, hivyo kushindwa kufanya shughuli za kimaendeleo.

Pia hali hiyo ya kukosekana kwa bidhaa, inasababisha wafanyabiashara hao kupata hasara kutokana na gharama mbalimbali wanazoingia.

Kwa ujumla, kuwapo kwa tatizo hilo kuna athari kubwa kiuchumi na kijamii. Hatua hiyo inasababisha kupanda kwa gharama za uendeshaji katika maeneo ya uzalishaji huku baadhi ya huduma zikipatikana kwa shida.

Suala hilo liko wazi kutokana na matatizo ambayo yaliwahi kujitokeza miaka kadhaa iliyopita pale mafuta yalipokosekana katika vituo mbalimbali hususan mkoani Dar es Salaam baada ya wafanyabiashara kutaka kupandisha bei ya bidhaa hiyo.

Hali hiyo ilisababisha magari mengi kutofanya kazi na hatimaye kukwamisha huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Pamoja na kilio hicho cha wafanyabiashara wa mafuta, kukosekana kwa fedha za kigeni hususan Dola katika mzunguko kuna madhara makubwa katika sekta mbalimbali zikiwamo za biashara.

Ni dhahiri kwamba Tanzania haizalishi bidhaa nyingi zinazotumika, zikiwamo nguo na viatu, hivyo wafanyabiashara hulazimika kuagiza nje ya nchi na sarafu inayotumika ni Dola ya Marekani. Kwa mantiki hiyo, kukosekana kwa Dola katika mzunguko wa fedha husababisha mkwamo kwa wafanyabiashara katika kuagiza bidhaa nje na matokeo yake hata mapato ya serikali hupungua.

Mapato mengi yanayokusanywa na serikali kwa kiasi kikubwa hutokana na kodi na ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoagizwa. Kwa maana hiyo, uagizaji bidhaa unapokuwa mdogo, serikali inashindwa kukusanya mapato yatokanayo na mizigo. Ukusanyaji mdogo wa mapato kutokana na mizigo kutoka nje husababisha miradi mbalimbali ya maendeleo kusuasua kwa sababu ya ukosefu wa mapato ya serikali.


Ni hali ya kutia matumaini kwamba serikali imekisikia kilio hicho na hatimaye kuchukua hatua za kukabiliana na tatizo hilo. Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, akizungumza na vyombo vya habari jana, alisema kwa kuanza, serikali imeachia dola milioni 20 katika mzunguko wa fedha ikiwa ni hatua ya kupunguza makali ya uhaba wa fedha hizo.

Licha ya kufanya hivyo, alisema serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pia imeanza kurejesha sehemu ya Dola ambazo zilichukuliwa mikononi mwa wafanyabiashara miaka kadhaa iliyopita huku pia ikifanya jitihada za kuwarejeshea leseni wamiliki wa maduka ya fedha za kigeni ambao walinyang'anywa kutokana na kutokukidhi vigezo.

Kwa ujumla, hatua iliyochukuliwa na serikali katika kukabiliana na uhaba wa Dola ni ya kupongezwa. Serikali katika hilo, imedhihirisha kuwa ni sikivu katika kuchukua hatua juu ya kero zinazowakabili wananchi wake, wakiwamo wafanyabiashara ili kukuza uchumi na ustawi wa wananchi.

Hata hivyo, ni vyema wafanyabiashara wenye mahitaji ya sarafu hiyo kwa ajili ya shughuli zao za kila siku, wakatumia fursa hiyo kutumia fedha hizo kwa njia zinazostahili na hatimaye kuleta matokeo chanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wanasiasa kosoaneni kwa uhuru wenye mipaka

Na Sabato Kasika

**MAKAMU** Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, amesema ingawa nchi ina uhuru mkubwa wa kusema na kutoa maoni, lakini ni vyema ukazingatia mipaka.

Kiongozi huyo alisema hayo jijini Dar es Salaam katika mkutano wa kitaifa wa wadau kujadili hali ya demokrasia nchini kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Mkutano huo uliandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), na kushirikisha wadau mbalimbali wa vyama vya siasa, huku hoja mbalimbali zikiibuliwa na wadau hao.

Miongoni mwa hoja hizo, ni hiyo iliyotolewa na Kinana kwamba anadhani uhuru wa kusema upo lakini kila uhuru una mipaka yake, huku akimkariri Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kwamba alikuwa akitufundisha kuwa uhuru bila ya nidhamu ni wendawazimu.

Akaongeza kumkariri kuwa nidhamu bila uhuru ni utumwa na kwamba kila uhuru lazima uwe na mipaka yake na kwamba uhuru upo wa kutosha, wakati mwingine labda kuna kasoro katika utekelezaji wake akifafanua kuwa ndio maana Watanzania wanapiga kelele katika kusimamia sheria zinazowapa Watanzania uhuru wa kusema.

Ninaungana naye katika la mipaka katika uhuru huo, kwani baadhi ya wadau hasa wanasiasa wamekuwa wakitumia lugha ambazo wakati mwingine zina ukakasi wanapowasilisha ujumbe kwa viongozi wa nchi.

Ingekuwa ni vyema wakazingatia mipaka, badala ya kutumia lugha ambazo zitatafsiriwa kuwa si za staha kwa viongozi wa nchi, badala yake wafikishe ujumbe wao kwa lugha nzuri wanayoweza kueleweka.

Kwa wale ambao wamekuwa wakiwafutilia wanasiasa kwenye mikutano ya hadhara wanayofanya, mjadala mkubwa umekuwa ni sakata la uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam.

Lakini ukosoaji ambao baadhi yao wamekuwa wakiutumia, ninadhani ndio umemfanya hata Kinana aseme uhuru unapaswa kuwa na mipaka, hasa baada kubaini kuwa kuna maneno yasiyofaa katika ukosoaji huo.

Binafsi ninaungana na Kinana katika hilo, kwamba suala la kuheshimiana ni la msingi kati ya viongozi walioko madarakani na wale wanaotafuta madaraka hayo, njia hiyo inaweza kuimarisha umoja.

Wanasiasa na wengine wasio wanasiasa wako huru kukosoa au kutoa maoni yao kwani ni haki kikatiba, lakini ingekuwa ni vyema kama wasingetumia maneno makali katika kufikisha ujumbe wao.

Ninadhani jamii yeyote itakayoshindwa kujali uhuru na mipaka, inawezza kijikuta si jamii bora, lakini vilevile kama itakapuuza uihuru wa watu wake na kuthamini mipaka zaidi jamii haitakuwa na furaha.

Ikumbukwe kuwa katika Jamii watu kuwa na uhuru usio na mipaka, kuna athari nyingi,kwani mtu anaweza kufanya kila ajisikiaolo na apendalo kulifanya bila kujali choachote, jambo ambalo si sahihi.

Hatua hiyo ya uhuru bila mipaka, inaweza kusababisha kuvunjwa na kuharibu heshima ya mtu mwingine, lakini pia uhuru bila mipaka unaweza kusababisha kuharibu mila na desturi nzuri za jamii.

Kwa maana hiyo, ingekuwa ni vyema kama wanasiasa watafanya shughuli zao kwa kuzingatia kwamba uhuru nao una mipaka yake, ingawa wengine hudai kwamba uhuru na mipaka ni utumwa.

Ninaamini kuwekewa mipaka lengo lake ni kuwafanya watu wa kawaida na hata viongozi wasivunjiane heshima badala yake washauriane, wakosoane lakini kwa kuzingatia uhuru wenye mipaka.

Wakati mwingine kitendo cha kutumia kauli au maneno makali katika ukosoaji, kinaweza kusababisha hata wale wanaomsikiliza mkosoaji kuachana naye na kuona kama wanapoteza muda wao bure.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Ifahamu Katiba ya Tanzania kwa jicho la mtunga Katiba



Pascal Mayalla

MAKALA hii ina lengo la kuwaelimisha Watanzania wenzangu hasa wale wa kawaida kuijua katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ya mwaka 1977 lakini kwa jicho la mtunga katiba.

Nikiwa mwandishi wa habari na wakili wa kujitegemea, nimeamua kujitolea kutoa bure elimu ya uraia kuhusu katiba. Hii ni kutokana na kupata bahati ya kufunzwa katiba na walimu nguli, wabobezi na wabobevu wa sheria na katiba.

Kupitia safu ya Kwa Maslahi ya Taifa, elimu hii itakuwa na mada zitakazofuatana ili kuwasaidia Watanzania wenzangu si tuu kuijua katiba ya nchi bali pia kuelewa mtunga katiba alidhamiria nini alipoweka kifungu fulani ili tutakapoanza mchakato wa katiba mpya, wananchi wengi wawe na uelewa wa katiba iliyopo na upungufu uliomo hatimaye kuwa na uwezo wa kutaka katiba bora zaidi .

Kwanza kabisa, jambo la kwanza tunalopaswa kufahamu ni kwamba Katiba ni mkataba kati ya watawala na watawaliwa. Kama ilivyo Biblia Takatifu au Qurani Tukufu, katiba imeandikwa kwa maandishi, hivyo kila anayejua kusoma na kuandika anaweza kuisoma. Lakini kwa bahati mbaya, si kila mtu ana uwezo wa kuisoma na kuielewa, hivyo kuna watu maalum ambao wanavisoma hivi vitabu vya dini na kuwaelimisha wengine. Kwenye dini mara nyingi ni viongozi wa dini na kwenye siasa ni viongozi wa siasa.

Hata hivyo, kama ilivyo kwenye dini, si watu wote wanaweza kuisoma Biblia au Qurani na kuelewa, kutafsiri na kuwaelewesha wengine. Ni kazi inayofanywa na wachache waliojaliwa uwezo huo ambao huitwa wahubiri. Hivyo hivyo, si wote wana uwezo wa kuisoma katiba, kuielewa, kuitafsiri na kuwatafsiria wengine.

Kwa kuwa nimejaliwa uwezo fulani wa kuisoma katiba na kuielewa kwa jicho la mtunga katiba alidhamiria nini, nimeamua kuitumia dhamira ya mtunga katiba kwa uelimishaji umma kuhusu katiba na dhamira ya mtunga katiba.

Kwanza tujiulize Katiba ni nini?. Katiba ya JMT ni kitabu kidogo chenye kurasa 43 na ndiyo kila kitu kuihusu Tanzania, hivyo hakuna yeyote aliye juu ya Katiba. Ndio msingi mkuu na mwongozo wa uendeshaji wa nchi. Sheria, taratibu na kanuni zote za kufanya kila jambo, lazima zitokane na Katiba.

Katiba yetu imeweka misingi mikuu minne ambayo ni uhuru, haki, udugu na amani. misingi hiyo inaweza kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo serikali yake husimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi na pia yenye Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo, hivyo kuhakikisha haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa pia wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu.

**KATIBA NI YA NANI?**

Katiba hii imetungwa na Bunge maalum kwa niaba ya wananchi kwa madhumuni ya kujenga jamii na kuhakikisha Tanzania inaongozwa na serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia. Kwa mujibu wa Katiba hii, kitu muhimu kabisa kwa taifa la Tanzania ni watu.

Kwa mantiki hiyo, Watanzania, hawa ndio wenye katiba. Kwa maneno mengine, Katiba ni mali ya Watanzania. Ni Watanzania ndio walioweka misingi mikuu minne ya katiba - uhuru, haki, udugu na amani. Msingi mkuu wa kwanza wa katiba yetu ni uhuru na wa pili ni haki, hivyo vitu vitu viwili vikuu vya Katiba yetu ni uhuru na haki.

Viongozi wakishachaguliwa kwa mujibu wa Katiba katika uchaguzi huru na wa haki, ulioendeshwa na tume huru ya uchaguzi, wanaapishwa kwa Katiba kutimiza majukumu yao kwa mujibu wa Katiba na kuilinda na kuitetea katiba ya JMT.

Kwa bahati mbaya sana, baadhi ya viongozi wetu, wengine wakubwa kabisa wako kwenye kundi la wasoma Katiba wasioielewa. Wanachaguliwa kwa mujibu wa Katiba wasioifahamu na waapa kuilinda Katiba wasioilewa na mwisho wa siku badala ya kuilinda wanakuwa wa kwanza kuivunja katiba bila kujijua kwa sababu hawajui watendalo kuwa ni kinyume cha Katiba!

Katika uendeshaji wa nchi, tuna mihimili mitatu ya Dola inayoendesha nchi yetu, mihimili hii ni Serikali, Bunge na Mahakama. Ili kuendesha nchi kuna watu muhimu ambao wanatajwa katika Katiba ili kuhakikisha inafuatwa na hawa ni wanasheria.

Wako wanasheria serikalini, bungeni na wanasheria mahakamani ambao ndio walipaswa kuijua Katiba lkini kwa bahati mbaya baadhi yao pia hawaijui katiba! Matokeo yake ni zinatungwa sheria batili na viongozi wa serikali wanavunja Katiba, Bunge linavunja Katiba kwa kutunga sheria batili.

Mahakama nayo yenye jukumu la kutafsiri Katiba na sheria. Chombo hiki kimesheheneza wanasheria nguli, wabobezi na wabobevu lakini baadhi yao wameingiwa na upofu. Katiba inavunjwa, mahakama ipo inaangalia tu kwa kusema “the court is not the custodians of the will of the people”!

Tukutane Jumapili ijayo tujuzane kuhusu maana ya Katiba ni sheria Mama na ina maana gani?

**Wasalaam**
**Paskali**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Malumbano ya uwekezaji sasa yamekuwa ndui



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Nami nilikuwa miongoni mwa tuliopitia mtihani huo wa chanjo tukiwa shule za msingi na mpaka sasa tuna makovu mabegani lakini ilitusaidia na kutuokoa dhidi ya ulemavu ambao ungetupata kama si chanjo hiyo.**

NDUI ni moja ya magonjwa yaliyosumbua sana miaka ya zamani wakati ambao kinga na tiba vilikuwa adimu kwa binadamu, hivyo kusababisha madhara makubwa.

Baadhi ya watu walipatwa na ulemavu wa kudumu kwani ugonjwa huo uliathiri ngozi na wakati mwingine kushambulia macho na kusababisha upofu. Dawa za jadi zilitumika kukabiliana nao lakini ziligonga mwamba.

Hivyo mpaka kinga kupatikana, muda ulikwishakwenda na idadi kubwa ya watu kuathirika na kupitia kipindi kigumu cha mateso yaliyosababishwa na ugonjwa huo, ulioonekana kuwa hatari katika baadhi ya jamii.

Hatimaye kutokana na maendeleo, ikapatikana suluhu ya kinga dhidi ya ugonjwa huo. Watu karibu wote walichanjwa kupitia kampeni maalumu zilizoendeshwa kwenye makazi na hata shuleni kwa wanafunzi.

Watu waliochanjwa ndui walionekana kuwa na makovu katika mabega ya kushoto na alama hiyo ikawa ndio utambulisho wa aliyechanjwa. Kwa kweli kampeni yake ikawa kama ilivyofanyika kwenye chanjo ya UVIKO-19.

Nami nilikuwa miongoni mwa tuliopitia mtihani huo wa chanjo tukiwa shule za msingi na mpaka sasa tuna makovu mabegani lakini ilitusaidia na kutuokoa dhidi ya ulemavu ambao ungetupata kama si chanjo hiyo.

Nimeikumbuka chanjo hii kutokana na mambo yanavyoendelea nchini hasa baada ya kuibuka mjadala wa uwekezaji wa kampuni ya Dubai Port World kwenye bandari.

Mjadala huu umekuwa mkali ukisumbua vichwa vya watu waliojigawa makundi mawili, ya wanaopinga mkataba wa uwekezaji huo na wanaounga mkono ingawa yote yanapenda uwekezaji kwenye bandari yetu/zetu.

Hakika mjadala na malumbano haya, vinazidi kuvuta muda na kuupoteza kwa kubishana na kuitana majina na hata wakati mwingine kutukanana bila sababu badala ya kutafuta suluhu.

Kama wazee wetu wangeendekeza kubishana juu ya ndui na kutupiana maneno bila kutafuta suluhu, ni dhahiri kuwa ingetafuna wengi na pengine Watanzania tusingekuwa tulivyo leo.

Suala la uwekezaji bandarini limetuzubaisha na sasa hatuwazi mengine zaidi ya hilo. Tunapelekana mahakamani na tunatoka misimamo ikiwa ni ile ile. Tumefikia sasa kutoa matamko ya kidini na kuibua mjadala mwingine.

Hivi sasa tunatoana macho kwa kugombezana kuhusu kuchanganya dini na siasa kwa sababu tu ya mjadala wa uwekezaji huo. Tunasahau kuwa dini na siasa havitengamani kadri zinavyotegemeana katika kumlea binadamu.

Tunasahau jinsi tunavyotumia madhabahu kujipatia umaarufu wa kisiasa, tunasahau jinsi tunavyosogea karibu na viongozi wa dini ili kufanikisha masuala ya kisiasa, tukiamini kuwa katika dini watu huamini zaidi ya kwingineko.

Angalia tunavyowatanguliza viongozi wa dini katika kila matukio yetu yawe ya kisiasa na hata kijamii tu, tukitaka watuombee ili mambo yetu yakae sawasawa.

Tunawaita viongozi wa dini kuliombea taifa letu ili liende sawa kutokana na siasa tunazofanya, hivyo tunaepukaje kuchanganya dini na siasa, huku tukiona wachungaji, maaskofu na hata mashehe wakizipa kisogo nyumba za ibada na kukimbilia kwenye siasa!

Mambo haya yasingetuibukia na kulaumiana endapo tungetulia na kuona ni jinsi gani tunaweza kukaa pamoja na kujadiliana kuhusu uwekezaji huu wa DP World nchini, badala ya kutaka kutoana ngeu wakati sisi ni ndugu na nchi ni yetu sote.

Hivi tulifikia wapi au tulifanya nini baada ya kumsikiliza Mkuu wa Nchi, Rais Samia Suluhu Hassan akitaka tukutanishe fikra za watu tofauti na kuziweka pamoja na kuchakata uwekezaji huu na kuja na msimamo mmoja?

Tunajisahaulisha kwamba Rais Samia alisema huko wapo wanaopinga ambao yawezekana wana mawazo na hoja nzuri, tuwakaribishe tukae nao tuwasikilize ili tuje na kitu cha kujenga Taifa letu.

Tumeacha na badala yake tunamfanya afikie hatua ya kusema mambo mazito, kuwa hatuna mtu mwenye msuli wa kuigawa wala kuiuza nchi, hata kuvuruga amani iliyopo. Na kweli, tusikubali wajitokeze wa kututunishia vijimisuli vyao na kutaka kutuvuruga.

Hakika bado tuna fursa ya kukaa pamoja waungaji na wapingaji mkataba na kuona wapi pana matatizo na wapi pa kurekebisha na kwenda pamoja hata kufikia kupata chanjo ya mjadala huu usiofikia ukomo.

Watanzania tuna hiari ya kuamua kuendelea na DP World au kuachana nayo, kama tunaona maji yameshaingiwa ruba na hatuwezi kuogelea tena, kwa sababu wawekezaji ni wengi tu duniani, na tunaweza kuwapata kama tunaona bado kuna ulazima wa kuwekeza bandarini.

**Alamsiki!**



Baadhi ya wanafunzi wa Darasa la Saba wa Shule ya Mwalimu Jk Nyerere, Awali na Msingi, wakiwa katika picha ya pamoja walimu, wakurugenzi, bodi ya shule hiyo pamoja na wageni maalum wakati wa Mahafali ya 25 ya shule hiyo yaliyofanyika shuleni hapo Mbezi Beach jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri alia mmomonyoko wa maadili waaswa kuacha kukumbatia tamaduni za kigeni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, amesema ni ukweli usiopingika kuwa hali ya mmomonyoko wa maadili inaendelea kuwa changamoto na kuwataka watanzania kuacha kukumbatia tamaduni za kigeni.

Akizindua tamasha la kitaifa la Utamaduni lililofanyika viwanja vya stendi ya zamani Mjini Njombe juzi, Waziri huyo alisema watanzania wanapaswa kurudi kwenye utamaduni halisi wa Mwafrika.

Tamasha hilo limebebwa na kauli mbiu isemayo, "Utamaduni ni msingi wa maadili tuulinde na kuuendeleza."

"Kauli mbiu inatutaka sote kwa umoja wetu tukemee vitendo vyote vinavyokinzana na utamaduni wetu, hivyo niwaombe sana tukemee, tulinde utamaduni, tudumishe utamaduni wetu, utamaduni wetu ndiyo utambulisho wetu," alisema.

Waziri huyo alisema tamaduni za Tanzania zina maadili lakini tamaduni za nje zinawatoa watanzania kwenye reli.

"Sisi tuna desturi zetu na tusipolinda tutatoka kwenye reli kwa hiyo lazima tulinde tamaduni zetu, tamaduni za nje nyingine hazitufai," alisema Dk. Pindi.

Hata hivyo, alisema kuwa huko duniani watanzania wametambulika kwa sababu ya utamaduni wao, ikiwamo Lugha ya Kiswahili, umoja, mshikamano, amani na utulivu.

"Kumbe kuna watu wanakesha kwa ajili ya kutunza amani, upendo ndiyo maana tunasema msione vinaelea. Nchi ya Tanzania haina dini kwa sababu wote ni wamoja," alisema.

# Biashara China, Tanzania yafikia tril. 20/-

**Na Gwamaka Alipipi**

TAKWIMU zinaonyesha biashara kati ya China na Tanzania kwa mwaka 2022 ilifikia Dola za Marekani bilioni 8.31 (Sh. trilioni 20) sababu kubwa ikitajwa kuwa mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara yaliyowekwa na nchi hizo.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika kongamano la miaka 10 la kujadili changamoto na mafanikio katika muongo mmoja wa ushirikiano kati ya China na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kupitia Mradi wa Ukanda Mmoja, Njia Moja (BRI) katika masuala ya amani, umoja na maendeleo.

Balozi Mingjian alisema mwaka 2022, China ilikuwa mwekezaji mkubwa Tanzania, kwa uwekezaji wa moja kwa moja mara mbili ya muongo uliopita wa mwaka 2003 hadi 2013.

"Biashara kati ya Tanzania na China kwa mwaka 2022 ilifikia Dola za Marekani bilioni 8.31, na ukuaji wake ni sawa na mara tatu ya muongo uliopita," alisema.

Akitaja miradi ya kimkakati ambayo China na Tanzania wanashirikiana ni ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP), Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Uganda kuja Tanzania (EACOP) pamoja na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano.

Kadhalika alisema China imetoa ufadhili wa masomo kwa Watanzania zaidi ya 2,000 kuimarisha na kukuza uhusiano wa elimu nchini.

"Kwa kipindi cha miaka 10 BRI imejenga urafiki kati ya Tanzania na China kwani uhusiano wa kimkakati umekuwa imara," alisema. Akizungumza katika kongamano hilo, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, alisema BRI imeboresha miundombinu ambayo imesaidia kukuza biashara kwa Ukanda wa Afrika Mashariki. Zungu alisema kutokana na hilo, nchi za Afrika zipo sehemu nzuri kutumia fursa zilizopo kwa nchi hizo na mradi wa BRI umeboresha uhusiano katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Richard Kasesela, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa CCM, alisema mradi wa BRI unafanya kazi nzuri katika ujenzi wa miundombinu.

"CCM inashukuru uhusiano uliopo kati ya China na Tanzania kwa sababu Mwalimu Julius Nyerere, alitufundisha uhusiano wa kuishi pamoja, hivyo ninatamani BRI iangalie namna ya kuunganisha miundombinu ya Afrika ili iwe rahisi kufikika," alisema.

# DC ataka shule kuweka mfumo wa ulinzi

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE zimetakiwa kuweka mifumo imara ya ulinzi ya namna ya kupambana na majanga ya moto ikiwamo vifaa vya kisasa vya kuzimia moto.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba, alisema hayo juzi kwenye mahafali ya 19 ya Shule ya Sekondari ya St. Anne Marie Academy, yaliyofanyika shuleni hapo, Mbezi, Dar es Salaam.

Alisema ametembelea shule hiyo na kujionea uzio eneo lote la shule na askari wa kutosha wenye mafunzo na uwezo wa kutumia silaha za moto, wakiwamo mbwa wakali kwa ajili ya ulinzi wa shule.

"Usalama wa watoto inatakiwa kuwa kipaumbele cha kwanza kwa hiyo ni vyema shule zingine nazo zikaiga mfano huu kwa kweli mmejidhatiti na hata likitokea lolote mnaweza kukabiliana nalo," alisema.

Komba alimpongeza Mkurugenzi wa Shule hizo, Dk. Jasson Rweikiza, kwa uwekezaji alioufanya kwamba ameisaidia serikali kwa kiasi kikubwa kuwapa Watanzania elimu bora tena ya gharama nafuu.

Alisema uwekezaji huo umesaidia kuongeza ajira kwa watanzania na kuwapongeza wazazi nawalezi wa wanafunzi wa kidato cha nne kwa kutimiza wajibu wao wa kuwalipia ada ili wapate elimu bora katika shule hiyo.

Mkuu huyo wa wilaya alisema amefurahi kusikia shule ina mradi wa ufugaji wa ng'ombe na kuku kwa ajili ya nyama na mayai ya wanafunzi.

"Pia nimeshuhudia maabara tano kubwa zenye vifaa vya sayansi kwa vitendo, maktaba mbili kubwa zilizosheheni vitabu vya kila aina na mazingira mazuri ya wanafunzi kujisomea," alisema.

Aidha, alisema ada ikiwa himilivu itatoa fursa kwa watanzania wengi kumudu kuwalipia ada watoto wao na hivyo watakuja kusoma hapo ili wapate elimu bora inayotolewa shuleni hapo.

Mkuu wa shule hiyo, Gladius Ndyetabula, alisema wamechukua tahadhari ya kujikinga na majanga ya moto wakati wote na alimhakikishia kuwa wanafunzi wa shule hiyo wako salama.

"Shule imechukua tahadhali ya kujikinga na ajali zitokanazo na moto tunao askari wazuri wenye uwezo na mafunzo ya zimamoto kama mlivyoona kila bweni na darasa pia kuna vifaa vya kuzima moto wakati wa dharura ya moto," alisema.

# MAISHA

AGOSTI 27, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*

Ukurasa 14



## ROSTI YA FIRIGISI

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Namna ya kusafisha dirisha la nyumba




## KATUNIKA

Ukurasa 16



# HERENI BILA KUWASHA SIKIO

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | 2 | 1 | 3 |
| 1 | 3 | 2 | 4 |
| 2 | 4 | 3 | 1 |
| 3 | 1 | 4 | 2 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | | G | O | N | G | A |
| A | | | | G | | M |
| N | | Z | A | O | | K |
| G | A | O | | J | A | A |
| A | | N | T | A | | N |
| Z | | G | | | | Y |
| O | G | O | P | A | | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


NOA, ARA, PUA, ALE, ELEWA, PICHA, AENDE, CHAPA, AHSANTE, NIPASHE

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

| | |
|---|---|
| TIMBA | SIMBA |
| LUKU | |
| TUNDA | |
| KATA | |
| PIMA | |




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

JOHN alikwenda sokoni kununua nyanya na mambo yalikuwa hivi.

John: Nyanya zinauzwa kiasi gani?

Muuzaji: Kilo shilingi 1500

Kijana: Nimeagizwa unisagie tunataka kwenda kula na chipsi nyumbani

Muuzaji: Kijana usitanie kazi za watu

Swali
Chaza inapatikana sehemu gani

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mbinu anazotumia ibilisi kutesa wanawake

KARIBU tena msomaji wangu niendeleze kuhusu mbinu anazotumia shetani kutesa wanawake. Moja ya mbinu ni kuwatupia roho ya uchawi kama tulivyojadili wiki iliyopita. Leo nakupa mbinu nyingine.

Majini mahaba ni dude lingine. Shetani anawashambulia wanawake wengi kwa kuwatupia majini mahaba. Hufanya juu chini kuwaongoza wanawake waolewe na majini. Wanawake wengi sana wanateseka sana na hawa viumbe.

Wapo wanawake wamezaa na majini mahaba. Wengine wana watoto wa majini.

Wengine walishalipiwa mahari na tayari zimeshakubalika katika ulimwengu wa majini. Wanawake wa aina hii wana matatizo makubwa sana katika ndoa zao za kimwili. Wapo wanaoamka na kujikuta wameshiriki tendo la ndoa na viumbe wasivyovijua pasipo kuwa na sababu yoyote.

Na wakati mwingine hupuuzia na kuhisi kuwa ni ndoto tu, kumbe siyo ni kitu halisi! Na pia zimekuwepo kesi nyingi sana za haya majini mahaba kuacha fedha za matumizi chini ya mto mara baada ya kufanya uharibifu kwa wanadamu.

Pia zimekuwepo kesi nyingi majini mahaba yanawapiga waume za watu kimwili. Pia baadhi ya wanawake wakijikuta wamelala na wafu. Majini haya hubaka wanawake. Kipo kipindi ulikuwepo uvumi kwamba kuna "Popobawa" anatesa watu usiku. Ni hawa majini hahaba.

Isitoshe, haya majini mahaba hufanya kazi na makahaba. Huvunja ndoa za watu na hufanya kazi wa waasherati. Ni majini ya ajabu, yana majivuno na kiburi. Yanahusika na kutenganisha ndoa za watu, watoto kutelekezwa, nguo za kushawishi wanaume. Pia yanahusika na kupata marafiki wabaya, kufanya watu wakatae kufanya kazi. Hujificha ndani ya viungo vya mwili wa mtu. Makahaba wengi ni wanawake waliopagawa na majini mahaba. Hawawezi kutulia na mwanaume mmoja.

Silaha nyingine anayotumia shetani ni kumpandikizia mwanamke roho ya upweke. Inawezekana kabisa mtu kuishi katika familia ya watu wengi, lakini bado ni mpweke. Mwanamke anaweza kuwa ameolewa lakini bado mpweke.

Mwanamke anaweza kuwa ana watoto wengi wamemzunguka lakini bado ana upweke mkubwa sana. Upweke ni mshale ambao shetani huutumia kushambulia wanawake.

Roho ya kuachika ni eneo lingine. Shetani hutumia nguvu za kutenganisha ndoa ili kumshambulia mwanamke. Zipo mbinu nyingi ambazo shetani anatumia kuwashambulia wanawake ili waachike.

Kama wanawake wangefunguliwa vinywa vyao na kuongea, ungeshangaa jinsi roho hizi za kuachika zinavyofanya kazi katika maisha yao.

Roho ya Yezebeli. Hii ni roho ya aina gani? Ni ile inayomfanya mwanamke atawale nyumba yake zaidi ya mume wake. Yaani inamfanya mwanamke awe na mamlaka zaidi ya mumewe.

Roho hii imevuruga sana na kuharibu maisha ya wanawake wengi. Wamejikuta wakiharibiwa na hii roho ya Yezebeli. Roho hii inapomvaa mwanamke anakuwa anataka kupewa heshima kuliko mumewe.

Wanawake wengine wenye hii roho, hufikia mahali kuwapiga waume zao kimwili. Na kwa sababu mwanaume ni kichwa, anapoona hali hii inaendelea ndani ya nyumba, huchukua maamuzi ya kutafuta wanawake wengine wa nje wa kumfariji, yaani nyumba ndogo.

Ni muhimu unapogundua unateswa na roho hii ya Yezebeli, tafuta msaada wa kiroho ili uweze kufunguliwa kutoka kifungo hiki ambacho kimesababisha ndoa nyingi kuvunjika.

Hii pia ni roho ya kuabudu sanamu. Humfanya mwanamke apende kufanya matambiko, mambo ya ushirikina akidai eti anamlinda mume wake na watoto, kumbe anawaunganisha kuzimu.

Roho zingine ni za ukoo na familia. Ni roho inayofuatilia familia kiasi kwamba ikianza kufanya kazi hushambulia kila mwanamke aliyetoka katika familia hiyo.

Zipo koo zingine zinafuatiliwa na laana za kuachika. Koo zingine ni za wake wengi. Kama hautazivunja hizi roho za ukoo, unaweza ukajikuta unapata matatizo makubwa katika ndoa.

Roho nyingine ni umasikini. Shetani anawaambukiza wanawake wengi roho ya umasikini. Ikishapandikizwa katika maisha ya mwanamke, matatizo mengine yanafuata.

Matatizo ya uzazi. Hii ni njia nyingine ya shetani kuwafanya wanawake wateseke na kila aina ya maradhi. Na kwa bahati mbaya magonjwa mengi ya wanawake hayatibiki hospitali.

Roho nyingine ni ya kukataliwa. Hii mwanamke hukataliwa kila aendako. Pia maagano ya kuzimu na afya mbaya.

***Tuishie hapa, fuatilia roho zaidi. Hadi wiki ijayo. Kwa maoni, ushauri, ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Malasusa anaijua KKKT, wasioijua hawana kifua

Alex Gehaz Malasusa, mmoja wa viongozi wabobezi na mahiri katika medani ya uongozi ndani ya kanisa , amechaguliwa tena kuwa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) katika mazingira tofauti ya kikatiba.

Mabadiliko ya katiba ya KKKT iliyoridhiwa na Mkutano Mkuu wa 21 wa kanisa hilo uliofanyika kwa takribani siku nne katika Chuo Kikuu cha Tumaini-Makumira kilichoko Usa River, mkoani Arusha, yamempa nguvu ya kurejea kuiongoza KKKT, ambayo kwa sasa ina kibarua kigumu cha kujenga umoja wa kanisa.

Nikiri wazi kwamba mimi ni muumini wa KKKT wa kuzaliwa na kurithi dini kutoka kwa baba. Bahati nzuri mama yangu pia ni mlutheri lakini haizuii mimi kueleza au kutoa maoni yangu juu ya misingi ya kanisa na namna ya kujenga umoja wa kanisa.

Kwanza, nianze kwa kumpongeza Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, kwa ushindi wa kishindo alioupata katika uchaguzi uliomrejesha kwa mara nyingine kuliongoza kanisa kwa miaka minne ijayo.

Askofu Dk. Malasusa, anarejea tena kwenye nafasi hiyo aliyoihudumu kuanzia 2007 hadi 2015, alipomaliza kipindi chake na kumpisha Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Frederick Shoo. Askofu Dk. Malasusa anachukua nafasi ya Askofu Fredrick Shoo, aliyemaliza muda wake wa uongozi wa awamu mbili.

Dk. Malasusa alipata ushindi wa kura 167, sawa na asilimia 69.3, huku mpinzani wake, Askofu Dk. Abednego Keshomshahara wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, akipata kura 73, sawa na asilimia 30.7

Tangu alipochaguliwa usiku wa Agosti 24, 2023, baadhi ya Watanzania na waumini wa KKKT, huko kwenye mitandao ya kijamii, wanasema ana kazi ya kuzitafsiri changamoto zilizoko ndani ya kanisa na kuzitatua.

Haya ndio mambo yanayomkabili Mkuu mpya wa kanisa; hasa mambo ambayo ni changamoto, kama utekelezaji wa katiba mpya iliyopitishwa na kanisa. KKKT ndio kanisa la pili kwa ukubwa Tanzania, nyuma ya Kanisa Katoliki, hilo halina ubishi.

Katika mitandao ya kijamii, mambo yanayoendelea huko ni ya kutizama, kupima na kujitathimini ni kwa namna gani anaweza mkuu mpya mteule wa kanisa akayafanyia kazi.

Kulaumu uchaguzi na kulaumu mabadiliko ya katiba ya KKKT, ni ukasuku lakini ni vyema busara ikatuongoza kuliko kutoa maoni ya kulaumu uchaguzi kwa sababu mjadala wowote hauwezi kubadili matokeo.

Askofu Dk. Malasusa, ndiye Mkuu wetu wa Kanisa kwa sasa mpaka mwaka 2027. Hilo liko wazi na halina ubishi. Anaijua KKKT. Msioifahamu KKKT rejeeni katika mabadiliko ya katiba.

Kama ndivyo, tutoe maoni ya kumsaidia Mkuu wa Kanisa Mteule ili aliongoze kanisa na kutuvusha salama hadi 2027. Najua wako wanaokubaliana na wako wasiokubaliana katika hili.

Pamoja na hayo, Askofu Malasusa aelewe mawazo ya waumini wake na hilo limpe chachu ya kubadilika. Si jambo la furaha sana unapochaguliwa kiongozi, halafu wale unaowaongoza wakaumia. Inatakiwa wafurahi.

Kama muumini na mzalendo wa kanisa na taifa langu, namsihi mkuu mpya wa kanisa, achukulie kwa umakini maoni yote yanayotolewa na ayafanyie kazi.

Ni ushauri tu. Najua ushauri unaweza kukubaliwa au kutokubaliwa. Unaweza kupokewa kwa mitazamo tofauti, yaani mtazamo hasi au chanya.

Askofu Dk. Malasusa, anza na kushughulikia tofauti za kimtazamo miongoni mwa maaskofu unaowaongoza. Jitahidi kujenga umoja wa kanisa, kuzileta pamoja mali na rasilimali za kanisa zilete umoja wa kanisa.

Iko wazi kwamba Askofu Dk. Malasusa, anakabiliwa na kibarua kizito cha kutatua tofauti hizo. Lakini pia liko suala la utekelezaji wa katiba moja, linaweza kuwa changamoto kwake, lakini usiogope, mtangulize Mungu mbele, busara na hekima.


Wewe ni mbobezi katika uongozi na sio mtu mpya katika kuliongoza kanisa la KKKT. Una kazi ya kufanya ili mali zote za kanisa, ziwe za umoja wa kanisa.

Tangu kuanzishwa kwa kanisa hilo nchini mwaka 1963, KKKT imeongozwa na Askofu Dk. Stefano Moshi, Dk. Sebastian Kolowa, Dk. Samson Mshemba, Dk. Alex Malasusa na Dk. Frederick Shoo.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI







AGOSTI 6, MWAKA HUU ILIKUWA SIKU YA KUKUMBUKWA KWA SULTAN RAMADHAN NA FAUDHIA AHMED BAADA KUAMUA KUFUNGA NDOA. HARUSI ILIFUNGWA NYUMBANI KWA WAZAZI WA BI HARUSI ENEO LA KIMARA MALAMBA MAWILI NA SHEREHE YA KUWAPONGEZA ILIFANYIKA YOMBO VITUKA JIJINI DAR ES SALAAM.





# MITINDO






# ABAYA NI ZAIDI YA VAZI

VAZI la abaya limepata umaarufu kwa wanawake wengi nchini, sio tu kwa kuhifadhi mwili, bali ni kutokana na unadhivu wake pale linapovaliwa.

Uvaaji wa vazi hili halihusishi na imani za kidini pekee, hata wale ambao wanahitaji kujihifadhi limegeuka suluhisho kwao.

Awali mavazi yaliyokuwa yakipendwa kwa kwa stara ni kama baibui, madera, magauni marefu ya kanga, vitenge na batiki. Lakini sasa vazi hili limeshika nafasi ya kipekee.

Vazi hili limepata umaarufu katika siku za hivi karibuni kutokana na kutengenezwa kwa mitindo mbalimbali ya kisasa.

Kwa sasa vazi hili linaboreshwa kwa kuwekewa nakshi, jambo linalofanya watu kuendelea kulivaa na kupata umaarufu.

Abaya ni maarufu kwa rangi nyeusi au rangi yoyote ya kung'aa linalofanana na baibui, ambalo linavaliwa juu ya nguo.

Vazi hili limekuwa tishio kutokana na kuuzwa bei kubwa tofauti na baibui na mavazi mengine ya stara.

Wavaaji wa abaya wamekuwa wakivutia watazamaji kutokana na kutulia kwenye mwili na linaloweza kuvaliwa na mtandio unaofanana rangi.

Kama ambavyo unaona kwenye picha vazi la abaya linavyovutia nawe unaweza kulivaa ili kwenda na mtindo mpya wa mavazi unaoendelea ndani na nje ya nchi.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# Hereni bila kuwasha sikio





KAMA kuna kitu kina kera ni pale unapovaa hereni baada ya muda mfupi masikio yanawasha.

Mbali na usumbufu huo wa kuwasha masikio kwa muda mrefu, kuna hili la sehemu zilizopita hereni kuanza kubadilika rangi na kuwa nyeusi.

Wakati mwingine masikio hupata maumivu makali, kuvimba na kutoa usaha.

Ukiwa kama mrembo unatakiwa kufahamu mbinu hii ya kusaidia kuvaa aina yoyote ya hereni bila kuwashwa wala kuleta shida yoyote kwenye masikio yako.

Ili kupunguza kuwashwa tunapovaa hereni zetu, ziko njia mbili ambazo ni rahisi sana na wala hazihitaji gharama kubwa.

Paka mafuta ya Vaseline

Mafuta ya Vaseline ni mazuri kwa kuzuia masikio kuwasha, kuzuia michubuko na athari za matumizi ya hereni kwenye masikio.

Tumbukiza hereni zako unazotaka kuvaa kwenye mafuta kisha vaa kama kawaida.

Unaweza nunua kopo dogo la vaseline ambalo unaweza weka kwenye pochi au mkoba ili unapoenda maliwato kujitengeneza tengeneza unarudia kujipaka mafuta.

Paka Colorless

Rangi ya maji ya kucha 'Colorless' unaweza kuitumia kupaka kwenye hereni zako na kuepuka kupata tatizo lolote la masikio kuwasha.

Paka 'colorless' kwenye hereni zako na ziache zikauke na kisha vaa na hutapata tatizo la kuwasha.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Rosti ya firigisi

FIRIGISI nacho ni kitoweo kama zilivyo nyama nyingine na ndio sababu unaweza kula na chakula kama wali, ugali, chipsi au chakula chochote.

**MAHITAJI**

Firigisi za kuku nusu kilo, karoti moja, nyanya nusu kopo

vitunguu maji kimoja kikubwa, tangawizi, kitunguu swaumu kijiko kimoja cha chai na pilipili hoho moja.

Limao nusu kipande, chumvi, curry powder nusu kijiko cha chai

turmaric nusu kijiko cha chai, chilli powder robo kijiko cha chai, mafuta chopped coriander.

**MATAYARISHO**

Safisha firigisi kisha zikate vipande vidogo vidogo. Zichemshe pamoja na chumvi, limao na nusu ya tangawizi na swaumu mpaka ziive.

Baada ya hapo kaanga vitunguu mpaka viwe vya brown kisha tia tangawizi na swaumu iliyobakia na kaanga kidogo kisha tia nyanya.


Zipike mpaka ziive kisha tia spice zote pamoja na chilli. Zipike kidogo kisha tia firigisi bila supu, kisha zichanganye vizuri na uzipike kidogo.

Baada ya hapo tia karoti na hoho na supu iliyobakia. Vipike pamoja mpaka viive na supu ibakie kidogo sana. Malizia kwa kutia coriander na uipue na hapo firigisi zako zitakuwa tayari kwa kuliwa.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Namna ya kusafisha dirisha la nyumba

DIRISHA ni moja ya vitu vinavyochangia kung`arisha nyumba. Lakini ili liendelee kuwa bora na kung`arisha nyumba lazima lisafishwe.

Endapo hutaweka kipaumbele katika jambo hilo, usishangae kuona mvuto wa nyumba yako unaanza kufifia kidogo kidogo na mwisho wake ukaichukia kabisa nyumba.

Usafishaji wa dirisha ni lazima uwe na muda maalum ambao hakuna jua kali.

Na hiyo ni kwa sababu unaposafisha wakati wa jua kali, maji unayomiminia katika dirisha lako hukaushwa hata kabla ya kupitisha sponji, hivyo itakuchukulia muda mwingi na pia haliwezi kung`aa vizuri na huacha ukungu.

Wakati unasafisha unatakiwa uwe pia na dawa maalum au kama unatumia maji si vibaya ukadondoshea kidogo vitone hata viwili vya maji maalum yenye mchanganyiko wa limau, maarufu kama 'vinegar'.

Baada ya hapo unalowanisha sponji yako au kitambaa laini kwa kuchovya



kwenye maji hayo na kuanza kusafisha katika dirisha lako.

Hakikisha unasafisha kuanzia juu kushuka chini ili uchafu wote utiririkie huko kwa sababu kufanya hivyo kutakuhakikishia kuwa hakuna uchafu utakaodondokea kwenye sehemu ambayo umeshasafisha tayari.

Kama eneo la dirisha unalotaka kusafisha ni chafu sana au kuna vumbi jingi au utando wa buibui, futa kwanza kwa kitambaa kikavu kabla ya kusafisha na maji. Uwe makini kuchunguza uchafu ulioko kwenye kona za madirisha yako.

Epuka sana kuweka maji mengi kwenye sponji au kitambaa unachotumia kusafishia ili yasimiminikie chini sehemu ambayo si ya dirisha, iwe ukutani au sehemu nyingine isiyohusika.

Hakikisha unasuuza na kukausha dirisha lako kwa kutumia kitambaa kikavu na laini na baada ya hapo rudia tena kwa ajili ya kuling`arisha.

Kama utakuwa na dawa maalum ya kusafishia, itapendeza zaidi kuipulizia kidogo katika dirisha lako huku ukifuta kwa kutumia kitambaa cha pamba ambacho hakitoi nyuzi.

Hakikisha dawa unayotumia kusafishia ni ile ambayo haiwezi kuharibu au kupausha mbao za dirisha lako.

Kama dirisha lako ni la kioo, hakikisha sponji au kitambaa ulichotumia kusafishia kioo ni tofauti na kile unachosafishia kwenye fremu ama kona za dirisha lako.

Katika maeneo ya fremu na kona, safisha kwa kutumia kitambaa kigumu zaidi ambacho kitabeba uchafu wote kwa sababu eneo hilo huhifadhi uchafu mwingi.

# Mbao inavyoshika kasi kwenye mapambo

**Na Restuta James**

UBUNIFU umeendelea kushika kasi kiasi kwamba ni kama hakuna kisichoweza kubuniwa au kutumika katika uvumbuzi.

Uchunguzi wa gazeti hili umebaini kwamba unaweza kuwa na vyombo vyote muhimu vinavyotokana na vitu asili kama miti.

Unaweza kuwa na sahani, bakuli, bilauri (glass), sinia, jagi, vijiko, vikombe, picha n.k vilivyochongwa kutoka kwenye mti na nyumba yako ikaonekana ya kisasa.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Amma Khan, anaiambia NIPASHE kwamba miti inatumika kutengeneza vyombo vyote muhimu pamoja na mapambo mengine.

Anasema kuanzia chooni na bafuni, hadi sebuleni na jikoni, mwenye nyumba anaweza kuamua kutumia mapambo hayo ambayo yanaleta mwonekano mzuri ndani na 'ukisasa' wa pekee.


"Kuna nakshi za picha tofauti tofauti na vyombo pamoja na mapambo mengine ambayo yanatengenezwa kwa mbao. Ni vitu vizuri sana vinavyonogesha mwonekano wa ndani," anasema.

Anasema kuna bidhaa za kisasa za kugawa chumba au kupunguza ukubwa wa eneo ambazo zinasaidia kuongeza mvuto.

"Kuna partition nzuri ambazo zinatengenezwa hapa hapa nchini na zinanogesha sana nyumba...tuna picha za miti ambazo tunapaka rangi kwa ubunifu wa hali ya juu kiasi kwamba mtazamaji anaweza kudhani ni mti halisi," anasema.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
'KWANI ALIYECHARAZWA BAO TANO ALILALA UWANJANI AU AJASAJILI?'
MIMI SIONGEI NA MTU BALI MUDA NDIO UNAOONGEA
KWA HIYO DOMO LAKO NDIO UMELIBATIZA JINA LINAITWA MUDA?
JUKWAANI
NAAMINI NDANI YA SIKU SABA, KUANZIA HAPO HAWATOVAA TENA KWA KUWA NIMEWAOMBA NA WEWE ENDELEA KUWASISITIZA KWA UPENDO
BABA... MIE NAKUELEWA TENA SANA TU! ILA KUNA AKINA 'TOMASO' KAZI WANAYO!
HABARI
JAMII
'KAMA KWELI SURA SIO ROHO NATAKA UNITHIBITISHIE KWA KUNISAIDIA HELA'
SIJUI NIMFANYEJE ILI ROHO YANGU IRIDHIKE!
JAMAA ANATANUA BARABARA NZIMA UTADHANI ANATAFUTA HESABU KAMA SISI WAKATI YEYE KAPAKIA MCHUMBA!
MUANGALIE MWENYE DALADALA ANAVYO-HANGAIKA KUTUPITA UTADHANI GARI YA MASHINDANO!
TENA UKIMFIKIA KARIBU KAA UBAVUNI TUMCHU-NGULIE KAMA KAPAKIA PISI KALI AU ANAJICHOSHA
AKILI YAKE IPO 'WALUWALU' KESHAPIGA MSUBA MUACHE AYATIMBE TUONDOKE NAE
JAPO NAKUNYWA KWA MFUKO WAKO LAKINI 'MKE ANAUMA SANA' SIO SIRI
NAKUNYWA HUKU NIMEFUMBA MACHO NISIKUONE UNAVYOUGULIA
UKIMFANYIA MWENZAKO FITINA ILI OFISI YAKE UKAE WEWE, UJIANDAE KUONA 'MALOLOSO KILA TAIM!' TOKA LINI PANYA AKAPIGA MLUZI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KAZI UKWENI MSHAHARA 'ASANTE'

HABARI KIMATAIFA

# Niger yawatimua mabalozi, yawapa saa 48 kuondoka

**NIAMEY,** NIGER
VIONGOZI wa kijeshi nchini Niger wametoa saa 48 kwa mabalozi wa nchi nne za Ulaya kuondoka haraka, wakati tishio la kuondolewa madarakani kinguvu likizidi kushika kasi.

Mabalozi waliotakiwa kuondoka nchini humo ni wa Ufaransa, Ujerumani, Nigeria na Marekani.

Hatua hiyo inakuja wakati tishio la kuvamiwa kijeshi na vikosi kutoka Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) likizidi kupamba moto.

Katika barua tofauti kwa serikali za nchi hizo, wizara ya mambo ya nje ya Niger ilisema uamuzi huo umetokana na hatua ya mabalozi wa nchi hizo kukataa mwaliko wa serikali kwa ajili ya mkutano uliofanyika Ijumaa.

Pia taarifa hiyo ilisema serikali hairidhishwi na hatua za serikali zao zinazokwenda kinyume na maslahi ya Niger.

Hata hivyo Ubalozi wa Ufaransa nchini Niger, umelikataa tangazo hilo ukisema kuwa hautambui mamlaka ya watawala wa kijeshi.

Uhusiano unazidi kuzorota kati ya utawala mpya wa Niger na mataifa ya Magharibi, pamoja na jumuiya ya ECOWAS.

Ufaransa imeunga mkono mara kwa mara wito wa ECOWAS kuvamia kijeshi na kurejeshwa madarakani kwa rais Mohamed Bazoum, ambaye alipinduliwa Julai 26, mwaka huu.

Ufaransa ina wanajeshi 1,500 nchini Niger ambao walikuwa wakimsaidia Bazoum katika vita dhidi ya wanamgambo wanaoendesha harakati zao za kijihadi.

Marekani pia ina wanajeshi 1000 wanaofanya kazi hiyo.

Ijumaa, ECOWAS iliwataka viongozi wa mapinduzi ya kijeshi, kufikiria upya msimamo wao na kushinikiza kurejeshwa kwa utawala wa kiraia, huku tishio la kutumia nguvu likiwa bado liko mezani.

Viongozi wa kijeshi pia wameonya dhidi ya uingiliaji kati wowote, wakishutumu ECOWAS kushirikiana na nchi ya kigeni kutaka kuivamia nchi yao.

**DW**



Wanajeshi wa mapinduzi wakiwa wamekusanyika mbele ya kambi ya Ufaransa mjini Niamey. **PICHA: AFP**

# Russia yathibitisha maiti waliokufa ajali ya ndege

**MOSCOW,** RUSSIA
SERIKALI ya Russia imethibitisha kupata miili 10 na kisanduku cheusi cha sauti katika eneo la ajali ya ndege inayodhaniwa kumuua mkuu wa wanamgambo wa Wagner, Yevgeny Prigozhin.

Taarifa hiyo fupi ilisema kazi inayofanyika ni upimaji wa kijenetiki ya molekuli ili kuwatambua watu hao.

Ndege hiyo ilianguka karibu na mji wa Moscow siku ya Jumatano, na kudaiwa kuwa bomu au kombora lilitumika kuiangusha. Msemaji wa Ikulu ya Russia, alikanusha madai kuwa Kremlin ilitoa amri ya kuuawa kwa Prigozhin akisema ni uongo.

Prigozhin ambaye wakati mmoja alikuwa mwandani wa Putin, aliongoza uasi dhidi ya Russia mwezi Juni. Rais Putin aliuelezea uasi huo kama ni haini, lakini alifikiana makubaliano kwa mamluki wa Wagner kujiunga na jeshi la kawaida la Russia kwenda nchini Belarus. Hata hivyo, kutokana na uasi huo, waangalizi wengi walimtaja Prigozhin, kama mtu anayetembea akiwa kama amekufa kwani Rais Putin hawezi kumsamehe mkuu huyo wa Wagner. Wakati wa mkutano wa Ijumaa na waandishi wa habari, msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov, aliambia BBC kwamba kulikuwa na uvumi mwingikuhusu vifo vya kutisha vya watu wote 10 katika ajali ya ndege ya Jumatano katika eneo la Tver, kaskazini-magharibi mwa mji mkuu wa Russia.

**BBC**

# Marekani yazishutumu Russia,China

**NEWYORK, MAREKANI**
Marekani imezishutumu nchi za China na Russia kwa kuzuia tamko la pamoja la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kulaani ufyatuaji wa makombora ya Korea Kaskazini.

Nchi hiyo imeelezea nchi hizo zinaipa kiburi Korea Kaskazini, kwa kuzuia tamko hilo la kulaani ikiwemo jaribio la wiki hii la urushaji wa satelaiti ya kijasusi angani.

Wakati wa mkutano wa dharura wa Baraza la Usalama, wanachama 13 kati ya 15, wote isipokuwa Russia na China walilaani jaribio la pili la kijasusi la Korea kaskazini katika muda wa miezi mitatu.

Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa Linda Thomas-Greenfield, alisema hilo linapaswa kuwa suala linalo waunganisha lakini tangu mwanzoni mwa 2022, Baraza hilo limeshindwa kutekeleza ahadi zake kwa sababu ya nchi hizo.

Aidha pia ameshutumu kitendo cha maofisa wa Russia na China kuhudhuria gwaride la kijeshi la Korea Kaskazini mwezi uliopita.

**DW**

## Kamanda wa ADF auawa

**KIVU KASKAZINI,** DRC
JESHI la Uganda limedai kumuuwa mmoja wa makamanda wa kundi la waasi wa ADF lenye mafungamano na wanamgambo wa dola la Kiislamu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa jana Ijumaa,ilisema, kamanda huyo aliyetambulika kwa jina moja la Fazul, alikuwa raia wa Tanzania na amekuwa akiendesha operesheni katika bonde la Mwalika kwenye mkoa wa Kivu.

Waasi wa ADF wamekuwa wakiendesha shughuli zao kwenye misitu mashariki mwa Congo kwa zaidi ya miongo miwili na wamekuwa wakifanya mashambulizi ndani ya nchi hiyo na wakati mwingine nchini Uganda.

Kundi hilo halikutoa taarifa yoyote kuhusu kifo cha kamanda huyo.

Uganda kwa kushirikiana na jeshi la DRC imekuwa ikipambana na makundi ya wabeba silaha kwa karibu miaka miwili sasa.

**DW**

## Gabon wapiga kura kumchagua rais

**LIBREVILLE,** GABON
WANANCHI wa Gabon wamejitokeza katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kumchagua rais katika uchaguzi mkuu uliofanyika jana, Rais Ali Bongo, aliyekaa madarakani tangu mwaka 2009, akitarajiwa kushinda.

Ushindi huo ni fursa ya kuongoza tena nchi hiyo baada ya kifo cha baba yake Omar Bongo, aliyetawala kwa miaka 42, wakati mwanawe akifikisha miaka 14 ikulu.

Mpinzani wake mkuu ni Albert Ondo Ossa ambaye pamoja na Bongo wanaongoza kinyang'anyiro cha wagombea 14 wanaowania nafasi ya juu katika taifa hilo dogo la Afrika ya Kati.

Ondo Ossa, profesa wa uchumi mwenye umri wa miaka 69 ambaye aliwahi kuwa waziri chini ya Bongo kutoka 2006 hadi 2009, alichaguliwa na upinzani kuwa mgombea wake mkuu siku nane tu kabla ya uchaguzi.

Bongo anatafuta muhula mwingine wa miaka saba, baada ya mwaka 2016, kupata ushindi mwembamba kwa kumshinda mpinzani wake Jean Ping kwa kura 5,500.

Kuelekea uchaguzi huo, rais Bongo amekuwa akisumbuliwa na changamoto ya kiafya baada ya kupata kiharusi Oktoba mwaka 2018, na kutoonekana kwa muda wa miezi 10.

Mwezi Januari mwaka 2019, alikabiliwa na jaribio la mapinduzi ya kijeshi.

**RFI**

SAFU

MAKALA

# SABABU KUTENGWA WANAUME UZEENI



Na Magabilo Masambu

**"Katika robo ya nne, watoto 63,244 walifanyiwa tathimini ya lishe, watoto 738 sawa na asilimia 1.16, walikuwa na utapiamlo, huku watoto 52 sawa na asilimia 0.08 walikutwa na utapiamlo mkali ilibidi wapatiwe matibabu na huduma za lishe kwenye vituo vya afya kwa kushirikiana na wadau wa lishe", amesema.**

KATIKA jamii yetu kumekuwa na dhana mbili kubwa kuwahusu wanaume. Moja ni wanaume kufa mapema, wajane ni wengi kuliko wagane. Dhana ya pili ambayo ndiyo msingi wa hoja ni juu ya baadhi ya wanaume kuonekana kunyanyasika katika familia kwa siku zao za uzeeni.

Baadhi yao wanalalamika kutopata matunzo bora kutoka kwa watoto wao na malalamiko haya yamekuwa yakiwaangukia kinamama kwamba wanawafundisha watoto wasiwahudumie baba zao. Sababu kubwa ambayo imekuwa ikitajwa ni kwamba kinababa hao hawakuwajibika katika kuwatunza watoto na sasa watoto wamefanikiwa wanataka kuhudumiwa, kwa maneno mengine wanataka kuvuna wasipopanda.

Dhana ya kwanza inatetewa na sababu nyingi zikiwemo za kibaolojia, kisaikolojia lakini zaidi inaelezwa ni kutokana na mizigo ya familia kwamba wababa wengi wanahangaika sana kuhakikisha familia zinasimama. Wako wanaopatia na wako wanaokosa na kuonekana hawajali familia na mwisho wa siku wakishindwa wanazikimbia.

Dhana ya pili inategemea baba alivyoshiriki katika familia toka awali na hapa mara nyingi wanaume wengi tumekuwa tukijisahau zaidi na kudhani kwamba upendo kwa watoto ni kutoa pesa za ada, kununua chakula na mavazi pekee kumbe watoto wanataka kutuona waziwazi tukishiriki. Mbaya zaidi kila hitaji tunawapatia kinamama wafanye kwa niaba yetu, hivyo watoto tangu wanakua, wanajua mama ndiye anayewapikia chakula, anawanunulia nguo, anawalipia ada. Sasa haya mambo huwa yanaleta shida, tukiwa uzeeni tunaonekana hakuna tulichoshiriki katika kutegeneza maisha yao.

Watoto wakila chakula, wanamwambia mama asante kwa chakula, akinunua nguo mama asante kwa nguo. Akilipa ada mama asante kwa ada ya shule lakini kumbe nyuma ya pazia fedha zote hizo unatoa wewe wataache kukutenga wakifanikiwa? Na bahati mbaya mama atie neno tu kwamba baba yenu alikalia kazi ya ulevi na wanawake, mimi ndiye niliyekuwa nahangaika na ninyi, hapo umekwisha. Watoto lazima wakuone takataka.

Kuna wakati tunaweza kuwalaumu kinamama bure. Ni kweli kwamba kuna nyakati hali inakuwa ngumu sana katika kuendesha maisha lakini ni ujinga kiwango cha lami kuwakimbia watoto na mke labda kama unakimbilia mahali kwenda kutafuta kwa ajili yao ili ukirejea uwe na kitu mkononi kuliko kutelekeza na baadaye siku zimeenda unarudi. Watakupokea tu kama baba yao lakini lazima ujue wataweka moja kichwani siku wakifanikiwa watakushughulikia.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Musa katika halmashauri ya wilaya ya Arusha, Justina Mugera, anashuhudia hiki nachoeleza. Anasema katika kata yake watu hulima tumbaku zaidi kuliko mazao ya chakula. Baada ya mavuno wanaume ndio wenye haki na dhamana ya kuuza na baada ya mauzo hawakumbuki hata kununua chakula cha familia na kusababisha watoto kukosa chakula jambo linalosababisha kupata utapiamlo.

"Kama ilivyo katika vijiji vingi Tanzania kinamama ndio wakulima na watunzaji wa mashamba lakini mazao yakivunwa, mama hahusiki na hana haki ya kujua fedha hizo zinakwenda wapi. Hali hii inasababisha familia kukosa chakula kwa sababu kwa baba ndiye mmiliki wa pesa, hakumbuki tena familia. Walio wengi hutelekeza familia kwa muda mrefu wakitumia pesa za tumbaku huko wanakokimbilia", amesema.

Kutokana na hali hii, wanaume wametakiwa kushirikiana na familia zao kuhakikisha zinapata chakula bora ili kukabiliana na changamoto ya utapiamlo hususani kwa watoto wa chini ya miaka mitano.

Hayo yameelezwa wakati wa kikao cha tathimini ya lishe cha robo ya nne katika mwaka wa fedha 2022/23 kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri ya Arusha. Katika kikao hicho kilichoongozwa na Ofisa Tarafa ya Moshono, Dominick Njuriwa, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, imeoneka baadhi ya kinababa hawashiriki katika malezi ya watoto badala yake kuwaachia kinamama pekee wakiteseka na familia jambo ambalo linasababisha watoto kukosa chakula na kusababisha kuwa na utapiamlo.

Akiwasilisha taarifa ya tathimini ya lishe, Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Arusha, Doto Milembe, alisema licha ya kuwa hali ya lishe inaendelea kuimarika ndani ya halmashauri hiyo, vijiji 14 kati ya 67 kwenye kata saba zina changamoto ya watoto wenye utapiamlo.

"Katika robo ya nne, watoto 63,244 walifanyiwa tathimini ya lishe, watoto 738 sawa na asilimia 1.16, walikuwa na utapiamlo, huku watoto 52 sawa na asilimia 0.08 walikutwa na utapiamlo mkali ilibidi wapatiwe matibabu na huduma za lishe kwenye vituo vya afya kwa kushirikiana na wadau wa lishe", amesema.

Joshua Mollel, mkazi wa kijiji cha Olchorovus Kata ya Musa, anawaasa wanaume wenzake wasizikimbie familia zao na hasa pale wanapopata malipo ya pesa za Tumbaku.

"Mimi nawashauri wenzangu, pesa zitokanazo na tumbaku wazitumie katika kuboresha familia zao maana tunahangaika kwa ajili ya familia. Sasa ikiwa tutapata pesa ndiyo tutelekeze familia? Tunafanya makosa makubwa ambayo baadaye yatatugharimu," anasisitiza.

Juliana John, mama wa watoto wanne, anashangazwa na tabia za wanaume kuwa wapole na wanyenyekevu pindi wanapokuwa hawana pesa, lakini wazipatapo tu wanakuwa na ratiba nyingi za ghafula. Haya yanatokea katika baadhi ya vijiji vya halmashauri ya Arusha, lakini kwa ujumla wake tatizo ni kubwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mume ampasha mke 'siwezi kuiba, kuua kwa ajili yako'*



Na Adam Fungamwango

KATIKA maisha ya ndoa kuna wanaume wakorofi ambao huwanyanyasa wake zao lakini pia wako baadhi ya wanawake ni pasua kichwa.

Kuna wanawake ambao wanataka kuishi maisha ya juu kuliko uwezo wao na kipato cha waume zao.

Hawa huwapeleka puta wanaume mpaka wanachanganyikiwa kwa madeni na mawazo.

Akienda nyumbani kwa shoga yake na kukuta kuna televisheni flati na yeye ana ya chogo, akirudi nyumbani atamkoromea mumewe kwa nini wanaishi maisha yale na mpaka lini. Ikiwa hivyo, atamwambia mumewe kuwa atashindwa kuishi pale.

Mke akikuta televisheni ya inchi 30 kwa jirani yake na yeye ana ya inchi 14, atakwenda kulalamika kwa mumewe hata kama hana uwezo huo.

Wanawake wa aina hii wanawayumbisha sana waume zao kwa kuwalazimisha kutaka kuishi kama wanavyoishi wenzao.

Mume wa shoga yake au jirani yake huenda ana uwezo mkubwa kutokana na kazi anayoifanya na kipato chake kikubwa lakini wako wanawake hawajali hili. Wanataka waume zao wafanye vitu vifanane na wengine.

Fenicha za ndani ziwe kama wao, chakula na vitu vingine kama vile mavazi anataka afanane na wenye waume wenye uwezo.

Kubwa kuliko yote siku hizi kuna michezo ya upatu na mikopo inayoitwa 'kausha damu.'

Umkute amejiingiza kwenye mikopo hiyo, akikopa kila mkopo unaokuja tena bila kuzifanyia biashara pesa anazopata. Badala yake atazitumia kwenye rusha roho, 'kigoma cha Uruguay', kigodoro akitunzana na mashoga zake mpaka pesa ziishe.

Kinachotokea hapo ni kwamba anashindwa kulipa pesa, wakopeshaji wanakuja kuchukua fenicha na hapo inabidi mwanamume apambane kwa yeye mwenyewe kuamua kulipa au kwenda kukopa pesa sehemu fulani kwa ajili ya kulimaliza kwanza deni hilo.

Kwenye jamii yetu, wako kinamama wa aina hii ambao badala ya kuwa msaada mkubwa kwa waume zao kwa ajili ya maendeleo, wanakuwa ndio maadui.

Mambo haya yamekuwa tangu enzi na enzi na wala isidhaniwe kuwa baadhi ya kinamama wa kisasa ndiyo wenye tabia hii.

Ukitaka kuamini hili hebu tuangalie mashairi ya wimbo wa 'Shauri Yako' uliopigwa na bendi ya Super Mazembe, iliyokuwa na maskani yake nchini Kenya.

"Nilikuelezeaga ooo mama Fatu wangu mama. Mapenzi ya kwetu haita-tawiana mama. Tabia yako na yangu haisikilizani ee. Unaona unaona sasa oomama, unaona unaona sasa oo Fatu eee. Unapenda kuvaa mimi sina namna ooo mama, unapenda kula vizuri mimi sina pesa oo Fatu ee.

"Niibe mali, sizoewei eee, niue mtu nipate dawa ya pesa. Niibe mali watanifunga. Niue mtu dhambi kwa Mungu baba, kama hunipendi, uende lote mama. Shauri yako, shauri yako ee, shauri yako, shauri yako eee, shauri yako uende lote Zena wangu, siwezi kuua mtu mama dhambi kwa Mungu baba ooo."

Kabla sijaendelea nataka nifafanue kuwa maana ya 'uende lote' ni uende moja kwa moja, kwa Kiswahili kizuri ni kwamba hamtaki tena. Wimbo huu umeimbwa kwa Kiswahili na wanamuziki wa Kikongomani, hivyo kuna baadhi ya maneno yenye Kiswahili cha Lubumbashi.

Jamaa anajivua gamba baada ya kuchoshwa na tabia za mpenzi wake anayependa maisha ya anasa, kula vizuri, kuvaa mavazi ya gharama wakati mwanamume uwezo hana.

Huyu jamaa wala hajataka kujisumbua, kaamua kuachana naye.

Kuna huyu mwingine aliyemwimba Marijani Rajabu kwenye wimbo wake wa 'Tamaa Mbele'.

"Jamani mimi naimba, naimba na masikitiko. Anisikitisha Mwajuma alivyo hana mapimo. Mwajuma anaelewa ya kwamba mumewe kipato chake kidogo, hivyo inawabidi ya kwamba waishi kufuatana na uwezo. Lakini sivyo anavyofanya Mwajuma, hajui kukosa wala kupata, tamaa nyingi kaweka mbele na mambo mengine yamemzidi kimo, ooo Mwajuma lo wacha tamaa, tamaa itakuponza.

"Hana hata huruma wala fikira hata kidogo, mume anampeleka mbio hadi hana raha. Kila kukicha nataka hili, jioni yake anataka kile, akiletewa basi hata shukurani hana, leo na kesho kasahau kila kitu, ooo Mwajuma pesa hupatikana na tabu.

"Wanaishi nyumba ya kupanga, kila mwezi ni kodi ya nyumba, watoto wanataka matunzo, Mwajuma wala habari hana. Akili yake kwenye urembo na mapambo, huchunguza mwenzangu leo kavaa nini, akiona kapata khanga, lazima na yeye akadai, hata kama mumewe yupo kwenye muwambo, atalazimishwa aende akakope, kama si hivyo nyumbani hakulaliki, malalamiko na maneno chungu tele.

"Bwana Mashaka wacha kulalamika ovyo kama amekushindfa mrudishe kwao, tizama maisha yako yalivyobadilika, mke anakupeleka pita hata nguo ya kuvaa huna, madeni hayaseki, kama kweli anakupenda aache mambo ya tamaa.

Mwisho wake utakuja kuiba Mashaka, mwanamke atakuponza, kila unachompa yeye hatosheki."

Mwanamke wa aina hii hana tofauti na ule mkopo wa 'kausha damu.'

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie kwenu-8

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HUYU amekuja kufanya nini hapa?" Lilikuwa ni swali la kwanza bila kumsalimia mdogo wake.

"Nimemwita mimi." Akajibu kwa kifupi na kwa sauti kavu.

"Kufanya nini we Catty, mbona mpana hivi kama boti la sinema?"

Ilibidi Catty amweleze kila kitu kilichotokea. Kutoka kumkuta chini ya mti jana, ugonjwa wake mpaka kumpa pesa ya kujitibia na kumwambia awe anakuja kula chakula hapo mpaka pale atakapojisikia vizuri, kupata nguvu na kuanza kufanya kazi zake kama zamani.

"Mdogo wangu utakuja kukaribisha vibaka hapa."

"We dada acha hizo, James tangu lini anakuwa kibaka, watu wote wa Kinondoni Moscow wanamfahamu, anafanya kazi mbalimbali na wakati mwingine za ndani ya nyumba yao sijawahi kusikia ameiba?" Akajibu Catty kwa hasira iliyomfanya dada yake atulie kidogo na kushusha pumzi.

"Au umemuelewa mdogo wangu, kama umemuelewa si useme tu!" Carry akasema huku akitabasamu.

Bado mdogo wake alimuangalia kwa hasira kidogo, halafu akamalizia kusema.

"Dada huyu naye pia ni binadamu, hebu angalia hana maisha mazuri, na tumefundishwa kwenye vitabu vitakatifu vyote kuwa tuwasaidie wahitaji, mtu kama huyu ukimsaidia na kumfariji akajiona ana thamani mbele za watu na wewe unabarikiwa na Mungu, hata milango yako ya riziki inafunguka. Unasemaje unampenda Mungu wakati binadamu mwenzako aliyeumbwa naye kama wewe unamchukia?"

"Hee, mdogo wangu umefika mbali, basi, ila mimi kwa hili usinishirikishe na lolote, litakalotokea ni lako."

"Kilichopo hapa ni kwamba nimemwambia awe anakuja kula asubuhi, mchana na usiku kwa siku zote ambazo hatokuwa anafanya kazi, mpaka apone na kupata nguvu za kufanya kazi ataacha kuja, labda kusalimia tu, mengine unayaongeza wewe."

James alisikia kama kuna malumbano kati ya ndugu hao, lakini kwa bahati mbaya au nzuri hakujua ulikuwa ni wa kitu gani.

Akadhania ni mambo yao wenyewe. Wala hakujua kuwa yeye ndiye chanzo. Akaendelea kunywa chai kwa raha zake.

Catty akatoka chumbani na kumkuta anaendelea kunywa.

"Usiondoke kabla sijarudi, natoka dakika 10 tu kuna kitu nakwenda kuchukua hapo mbele, narudi sasa hivi,"




**"Kilichopo hapa ni kwamba nimemwambia awe anakuja kula asubuhi, mchana na usiku kwa siku zote ambazo hatokuwa anafanya kazi, mpaka apone na kupata nguvu za kufanya kazi ataacha kuja, labda kusalimia tu, mengine unayaongeza wewe."**

"Poa dada hakuna neno."

Carry ambaye yeye ndiyo alikuwa anatoka kazini kwenye shifti ya usiku alitoka naye chumbani na kumkuta James.

"Eeee, unakunywa tu chai kama nyumbani kwako. Baba mwenye nyumba!" Carry alianza kwa mzaha ili kumkera James.

"Unafikiri kila mtu ana roho mbaya kama wewe!" Akajibu jibu ambalo Carry hakulitegemea.

"We! Unanijibu hivyo mimi! Humu ni kwetu nimepanga na mdogo wangu wote tunatoa pesa ya kodi na chakula, nitakutimua sasa hivi!"

"Hapa nimekaribishwa na Catty na mimi siondoki, kasema mwenyewe hadi arudi."

"Ahaa kumbe Catty ndiyo anakutia kiburi eee, ngoja aje, nakufukuza na yeye yupo!" Akaongea kwa hasira

"Sikiliza wewe! Ukithubutu kunifukuza na yeye yupo hutoamini macho yako kitu ambacho nitakifanya! Usidhani siku zote nakuachia unanisema. Nakuachia kwa sababu mimi ndiyo nakuanza. Mimi ndiyo nakufuata kukwambia nakupenda. Kwa hiyo una haki ya kunijibu chochote, ingawa si vizuri kunidharau, kunitusi, kunidhihaki kama unavyofanya. Una haki ya kunikutaa au kukubali. Na mimi nina haki ya kuendelea kukubembeleza au kuacha. Lakini hili unalitaka kulifanya leo huna haki nalo hata chembe."James aliongea kwa sauti ya mamlaka iliyoonekana kumshtua na kumtisha Carry.

Amezoea kumchamba lakini hakuna hata siku moja amejibiwa kama hii leo. Akatulia kidogo. Lakini akajitutua."Ina maana unataka uugulie hapa?"

"Nani aliyekwambia naugua?"

"Unafikiri sijui, unaumwa, hela huna, huna pesa ya matibabu, huna pesa ya kula, kwa hiyo hapa ndiyo umeona sehemu ya kuja kuugulia. Yaani hapa ndiyo wodini, hotelini, halafu ndiyo unanitaka mimi." Akacheka kicheko cha kejeli.

"Sasa si ningekuwa na mzigo tu hapa, mtu anaumwa hata pesa ya matibabu inakushinda."

Maneno ya kejeli ya kashfa aliyokuwa akiongea Carry yangeweza kumuinua yeyote ambaye mwenye roho ndogo na tabia ya kususa.

Angeacha chai na kuondoka zake. Lakini haikuwa kwa James. Kitu kilichosaidia pamoja na kwamba hata tabia hiyo, alimfahamu Carry jinsi alivyo.

Hakumjibu, akaendelea kunywa chai na vitafunio vyake.

"Uroho tu."

"Sawa" Akajibu.

"Unataka uwe unakuja hapa kula huku unaumwa halafu ukizidiwa utufie tupate kazi ya kusaka ndugu zako ambao hatuwafahamu. Kafie kwenu." Carry akaendelea.

Catty aliingia na alionekana kama alisikia baadhi ya maneno, akauliza."Kuna nini?"

"Hakuna kitu." Carry akajibu haraka haraka na aibu.

Jicho ambacho mdogo wake alimtazama dada yake, akagundua kabisa kuwa alisikia baadhi ya maneno aliyokuwa anaongea na James.

Upesi upesi, akanyanyuka kwenye kochi na kuingia chumbani. Akatoka baada ya dakika 20 akiwa amebadisha nguo. Alikuwa ameacha dada yake chumbani. Akatoka na kumtazama James kwa jicho kali. Akaongea maneno ambayo hayakutakwa kwa sauti. Akaongea karibu yake kwa kuchezesha mdogo kimsisitizo. "Toka, kafie kwenu." Hakutaka kuongea kwa sauti akimuogopa mdogo wake. halafu huyo akatoka na kumcha, akafunga geti kwa nguvu.

James alikuwa ameshamaliza kula. Akabaki kimya akiangalia tamthilia iliyokuwa ikiendelea kwenye luninga.

Dakika 15 baadaye Catty alitoka chumbani. "Naona umeipenda huyo tamthilia." Akamshtua.

Akatabasamu halafu akajibu. "Ni kweli nzuri sana ila mimi mara nyingi sina muda wa kuangalia sana haya mambo."

"Vipi huyu mwehu ameshatoka!"

"Kaondoka kapita kanuna utafikiri kalazimishwa kuolewa na mwanaume asiyempenda."

Catty akaangua kicheko. "Kha! usinichekeshe mie James, kumbe una maneno hivyo. Vipi alipoondoka alikwambia kitu gani?"

"Hapana, hajaniambie kitu chochote, katoka vimbisha domo tu hapa." Akaongopa.

Ni kweli alitoka amenuna, lakini James hakutaka kumwambia ndugu yake kuwa dada yake amemwambia 'Kafie kweni.'

Pamoja na yote, James pia na busara. Hakutaka kuwagombanisha ndugu hao. Hakutaka wagombeni kwa ajili yake. Yeye ni mtu wa kupita. Ni mpita njia, anasaidiwa na muda na muda si mrefu ataanza maisha yake ya siku zote na hatofika tena pale. Kwa nini aondoke hapo na kuwaacha na ugomvi?

Alitaka wandelee kuwa na amani na undugu wao kama kawaida. Akajua yeye akiwa ndiyo sababu ya ugomvi wa ndugu hao, baadaye wote wanaweza kumchukia.

"Na yale aliyokuwa akiongea wakati mimi nimetoka?"

"Catty, si unamfahamu ndugu yako? Wewe acha tu, yeye anaongea mradi anajifurahisha, we unadhani mimi ndiyo kwanza nayasikia hayo maneno yake? Mimi hapa nimekufuata wewe mhisani wangu tu basi. Yeye na mimi tunamalizana wenyewe tu mbele ya safari huko."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# HEMANT PUNJABI KUWANIA SHINING STAR AFRICA AWARDS

Mwanamuziki mwenye asili ya India anayeishi nchini Benin, amefanikiwa kuingia kwenye tuzo kubwa barani Afrika za The Shining Star Africa zitakazofanyika Afrika Kusini mwezi unaokuja.

Punjabi anayetamba na wimbo 'Rock Your Body', amesema tuzo hizo ni tukio adhimu lenye kusherehekea mafanikio katika nyanja za sanaa ndani ya Afrika.

"Tuzo hizi zinaonyesha uwezo wa kujieleza kwa wasanii katika kuziba mapengo ya kitamaduni yaliyopo kwenye kizazi hiki na kukuza hali ya umoja miongoni mwetu. Najisikia fahari kushiriki tuzo hizi, naamini ni muda mzuri kwangu wa kutangaza albamu yangu mpya ya From India To Africa (FITA)," amesema Punjabi.



# MIKOSI INAMWANDAMA

MIKOSI bado inamuandama mwimbaji mkongwe kutoka Marekani, R Kelly, baada ya kiasi kikubwa cha pesa kuzuiliwa kwa ajili ya kuwalipa waathiriwa.

Mahakama imezuia kiasi cha dola 500,000 sawa na shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kuwalipa fidia wanawake walioathirika na vitendo vya unyanyasaji wa kingono uliofanywa na msanii huyo.

Kulingana na hati za kisheria zilizopatikana na TMZ, jaji alitia saini amri ambayo R Kelly atatoa kiasi hicho kutoka kwenye malipo ya mirabaha ya nyimbo zake baada ya kupatikana na hatia kati ya kifungo chake cha miaka ishirini kwa uhalifu wa kingono.

Inavyoonekana, kampuni ya Universal Music Group ilishikilia mirabaha yake mingi na ilikuwa bado haijalipa kiasi hicho kwa ajili ya kuwalipa waathiriwa, na ilibidi mamlaka ya kisheria kuingilia kati.

Aidha, ripoti zinaeleza kuwa sehemu kubwa ya mirabaha hiyo ambayo haijalipwa inatokana na vibao vya zamani vya msanii huyo wa R&B ambavyo UMG walikuwa hawajalipa hasa.

Kampuni hiyo ina zaidi ya dola 567000 ya mirabaha.

Nafasi ya mwanamuziki huyo mwenye miaka 56 ya kurudi kwenye ulimwengu wa muziki inaonekana kuwa ndogo kwa sasa.

Ingawa wengi wanamuunga mkono katika suala la kuendelea kusikiliza na kusifia muziki wake, wanakiri kwamba mambo yamekwenda mbali na mikosi bado inamuandama.

## ZISIKUPITE

### BALOGUN AKARIBIA MONACO
MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Folarin Balogun anakaribia kuhamia Monaco kwa pauni milioni 35 licha ya Chelsea na Inter Milan kumnnyatia.

### SANTOS ATUA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest imemsajili kiungo wa kati wa Brazil, Andrey Santos kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Chelsea. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye ameichezea mara moja timu yake ya taifa, alijiunga na Chelsea kutoka Vasco da Gama Januari kabla ya kutolewa tena kwa mkopo Machi.

### KUDUS AKOMALIWA
KLABU ya West Ham ipo kwenye mazungumzo na kiungo wa Ajax, Mohammed Kudus kuhusu uhamisho wa kitita kikubwa cha fedha. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alifunga hat-trick katika ushindi wa Ajax katika mchujo wa kuwania kushiriki Ligi ya Europa dhidi ya klabu ya Ludogorets nchini Bulgaria Alhamisi.

### TIERNEY HUYO SOCIEDAD
BEKI wa Arsenal, Kieran Tierney anatarajiwa kujiunga na Real Sociedad kwa mkopo wa msimu mzima. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland mwenye umri wa miaka 26 amecheza zaidi ya mara 120 akiwa na washikabunduki hao tangu ahamie kutoka Celtic mwaka 2019, lakini alianzishwa mara sita tu katika Ligi Kuu ya England.

### HAZARD AWANIWA
KLABU ya Crystal Palace inapanga kumjaribu mchezaji huru wa Ubelgiji, Eden Hazard kwa kumpa fowadi huyo wa zamani wa Chelsea na Real Madrid mwenye umri wa miaka 32 mkataba wa mwaka mmoja kule Selhurst Park licha ya majeraha yake. (***Football Transfers***)

### LIVERPOOL YAGOMEWA
OFA ya Liverpool ya pauni milioni 25.6 kwa ajili ya kiungo wa Brazil, Andre mwenye umri wa miaka 22, imekataliwa na Fluminense ambao wanasitasita kumuachia mchezaji huyo kabla ya kumalizika kwa msimu wao wa ligi Desemba. (***ESPN***)

### CITY NA PAGUETA
MANCHESTER City huenda wakafufua nia yao ya pauni milioni 80 kumsajili kiungo wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 25 Januari, mara tu uchunguzi wa Chama cha Soka kuhusu madai ya ukiukaji wa sheria ya kamari ya mchezaji huyo kukamilika. (***Sky Sports***)

### GABRIEL HAPATIKANI
ARSENAL wamewafahamisha wawaniaji wa Saudi Arabia na Real Madrid kwamba mlinzi wao Mbrazil, Gabriel mwenye umri wa miaka 25 hapatikani. (***Mirror***)

### LUKAKU ANUKIA ROMA
KOCHA mkuu wa AS Roma, Lina Souloukou amesafiri kwa ndege hadi London, na hivyo kuchochea uvumi wa mazungumzo na Chelsea kuhusu mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30. (***Tuttomercatoweb***)

### ODOI BASI TENA
KLABU ya Everton imejiondoa katika mpango wa kumnunua winga wa Chelsea na Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 22. (***Liverpool Echo***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POCHETTINO AMTABIRIA STERLING UFUNGAJI BORA

**LONDON,** England

**●●● Asema anastahili sifa kwa kiwango anachokionyesha, baada ya kuwa na wakati mgumu msimu....**

MAURICIO Pochettino alimmiminia sifa Raheem Sterling ambaye alianza kuonesha nia yake ya kuwa mfungaji bora wa Chelsea msimu huu kwa kufunga mabao mawili dhidi ya Luton, Ijumaa.

**Sterling aliendelea na mwanzo wake mzuri wa kampeni kwa mabao yake mawili na pia alipiga krosi ambayo Nicolas Jackson alifunga bao la tatu kwa Chelsea huku timu hiyo ya Stamford Bridge ikipata ushindi wa kwanza wa ushindani chini ya Pochettino wa 3-0.**

Sterling hakuwa na kipindi kizuri katika kikosi cha Chelsea kufuatia uhamisho wake wa pauni milioni 47.5 kutoka Manchester City lakini amefanikiwa wakati huu.

Pochettino alisema: "Anastahili sifa kamili kwa uchezaji wake. Nimefurahishwa sana naye kwa sababu aliniambia kuwa ulikuwa msimu mgumu kwake msimu uliopita na ninafurahishwa sana mchezaji anapofurahi na wakati mchezaji mkabaji anaweza kufunga na kutoa pasi, kwetu sisi ni hisia nzuri zaidi."

Naye Sterling alisema: "Ni lengo nililoliweka kuwa mfungaji bora wa Chelsea msimu huu, ni jambo ambalo najua ninaweza kufanya. Ikiwa ninafanya kitu kwa asilimia 100, najua ninachoweza kufanya na ndicho ninachofanya mwaka huu."

Bao la Jackson lilikuwa zawadi inayostahiki kwa kufanya kazi kwa bidii kutoka kwa ujio wa majira ya joto wa pauni milioni 32 na Pochettino alisema: "Ni mzuri. Ni ngumu kupata mchezaji kama yeye sokoni.

"Kwangu ana uwezo wa kuwa mmoja wa washambuliaji wakubwa kwenye Ligi Kuu England. Ni yeye pekee anayehitaji muda na si kuharakisha naye."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
NEWCASTLE
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 2.17
X | 3.86
2 | 3.03

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Sifaeli Nassr - 0652 736 XXX
2. Juma Seni - 0653 093 XXX
3. Saidi Yakuti - 0653 113 XXX
4. Joyce Nziku - 0672 719 XXX
5. Mesaidi Mbwana - 0672 862 XXX
6. Faya Kisusi - 0672 919 XXX
7. Raphael Shtam - 0674 595 XXX
8. Ezekiel Ezekiel - 0676 198 XXX
9. Jackson Diomedes - 0677 828 XXX
10. Makame Makame - 0779 322 XXX

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA ATAKA DIRISHA LA USAJILI LA SAUDIA LIFUNGWE MAPEMA

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ametaka dirisha la uhamisho la wachezaji la Saudi Arabia lifungwe sawa na la Ulaya - huku akishindwa kukataa kuwauza wachezaji zaidi ya Septemba 1.

Baadhi ya majina makubwa ya soka yamehamia Saudi Arabia msimu huu wa joto huku uwekezaji wa PIF katika klabu nne kubwa nchini humo ukiruhusu ongezeko kubwa la ada ya uhamisho.

Dirisha la usajili la Ligi Kuu ya England litafungwa Ijumaa ijayo lakini klabu za Saudia zitaweza kusajili wachezaji wapya hadi Septemba 20, jambo ambalo Arteta anaamini linahitaji kushughulikiwa.

Alipoulizwa kama wiki mbili na nusu za ziada za kumaliza biashara zitakuwa za haki, Mhispania huyo alijibu: 'Hapana, kwa sababu ni mshindani sasa. Hapana, nadhani tunapaswa kubadili hilo.'

Alisema kama tarehe ya mwisho ya usajili wa Ligi ya Saudia inapaswa kuendana na ile ya Ulaya.

"Ni mshindani mwingine na huleta fursa zingine kwa wachezaji, kwa wasimamizi na watu wanaofanya kazi kwenye tasnia kuamua.

"Mwishowe, tuko huru kuamua ni lini klabu, wachezaji au yeyote anatakiwa kukubaliana na jambo fulani, lazima uwe na nia ya kwenda kutafuta makubaliano, ndiyo maana kuna mikataba.

"Ikiwa watu wanakubali kwenda ni kwa sababu mtu anakubali kwenda huko, lakini mtu fulani alikubali kumuuza, kwa hiyo huenda kwa njia mbili au tatu tofauti."

Hakuna mchezaji wa Arsenal ambaye ameelekea Mashariki ya Kati msimu huu wa joto, lakini klabu za Saudia zimeripotiwa kutaka kumnunua Gabriel Magalhaes na Thomas Partey.

Ingawa anataka kuona tarehe ya mwisho ya kuhama kwa sawa, Arteta alisita kusema Arsenal itakataa kuwauza wachezaji baada ya dirisha la Ligi Kuu ya England kufungwa Septemba 1.

"Sawa, kanuni itakuwa kwamba (hatutazingatia ofa)," alisema.

"Lakini siwezi kufanya uamuzi kwa klabu. Ni watu wengi wanaohusika katika mchakato huo na wangekuwa na hakika ya kusema, umiliki, ungefanya vivyo hivyo.

"Itakuwa kwenye meza kama ofa yoyote na lazima uiangalie. Kitu pekee ninachosema sio bora kwa sababu wao ni washindani.

# Lukaku kupelekwa Roma kwa mkopo

**LONDON,** England

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo na AS Roma ya Serie A juu ya uwezekano wa kumpeleka kwa mkopo mshambuliaji Romelu Lukaku, kwa mujibu wa 90min.

The Blues hawakutaka kumtoa kwa mkopo mapema msimu huu wa joto kwa matumaini ya kupata mnunuzi wa kudumu wa Lukaku, lakini Mbelgiji huyo alikataa nafasi ya kuhamia Saudi Arabia na kuona Inter ikimaliza nia yao baada ya kujua mazungumzo ya Lukaku na Juventus.

Wakati Juventus wakiwa tayari kumsajili Lukaku moja kwa moja, ofa pekee zilizowasilishwa hadi sasa zimekuwa kama sehemu ya mpango wa kubadilishana na Dusan Vlahovic ambapo Chelsea pia italazimika kulipa ada ya ziada.

Baada ya kukataa tena kuhamia Saudi Arabia katika siku za hivi majuzi, wanunuzi wa kudumu wa Lukaku ni vigumu kupatikana na sasa 90min inaelewa kuwa Chelsea iko tayari kumwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kuondoka kwa mkopo.

Nia ya haraka imesajiliwa kutoka kwa Roma, ambao wanatafuta mbadala wa Tammy Abraham ambaye ni majeruhi.

Vijana wa Jose Mourinho walikuwa wameuliza kuhusu kumsajili Mason Greenwood kutoka Manchester United, lakini wanaona mtu aliye na uzoefu mkubwa kama Lukaku Serie A kama uhamisho salama zaidi.

Juventus wanalenga kumuuza Moise Kean na hawaamini kwa sasa watakuwa na nafasi ya kumsajili Lukaku hata kwa mkataba wa mkopo.

Kuvutiwa kwao na Mbelgiji huyo kunategemea kumuuza Vlahovic lakini hilo halionekani kuwa linawezekana kwani dirisha la usajili linaingia wiki yake ya mwisho.

Wawakilishi wa Lukaku wanafahamika kuwa waliwasiliana na klabu chache kuzijulisha kuwa anapatikana kwa mkopo.

Ripoti zimeitaja Paris Saint-Germain kama moja ya klabu zinazoweza kumtaka, ingawa Lukaku hakuwa na nia ya kuhamia mji mkuu wa Ufaransa mapema msimu huu wa joto.

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# KOCHA AZAM ASHUSHA LAWAMA KWA WACHEZAJI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuondolewa kwenye Michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na klabu ya Bahir Dar Kenema ya Ethiopia, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo amesema wachezaji wake hawakufuata maelekezo yake katika mchezo huo na kujikuta wakiyaaga mashindano hayo mapema.

Dabo alisema hakufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji na kucheza tofauti na vile alivyowaelekeza katika uwanja wa mazoezi.

Azam FC imekuwa timu ya kwanza kwa Tanzania kuondolewa kwenye michuano ya kimataifa mwaka huu baada ya kukubali kichapo cha mikwaju ya penati 4-3 kutoka kwa Waethiopia hao baada ya kukamilika kwa dakika 90 wakiwa na uwiano wa mabao 3-3.

Licha ya Azam kushinda mchezo wa juzi mabao 2-1 hayakutosha kuwavusha ndani ya dakika 90 kutokana na kukubali kipigo kama hicho kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Ethiopia na hivyo kulazimika kuingia kwenye mikwaju ya penalti.

Akizungumza na Nipashe jana, Dabo alisema hakutarajia kupata matokeo hayo kwa sababu walifanya maandalizi mazuri na matarajio yao ilikuwa kumaliza mchezo katika dakika 90 na kupata matokeo mazuri.

Alisema wachezaji wake hawakuwa makini katika mchezo huo kwa sababu hawakufanya kile ambacho aliwaelekeza kwenye uwanja wa mazoezi ikiwemo kupiga mipira ya kutenga ikiwemo Penati.

"Hatukuwa makini kwa sababu baada ya kupata bao mbili kipindi cha kwanza tukaridhika mapema na tulipoteza umakini kwenye nafasi tulizozitengeneza, lakini pia katika upigaji wa mipira ya kutenga na upigaji wa penalti.

"Sina presha juu ya kushindwa kusonga mbele, wapinzani wetu (Bahir Dar Kenema) walitumia nafasi walizopata na kufanikiwa kufunga bao la kwanza na dakika 90 kukamilika tukiwa jumla ya mabao 3-3, tukashindwa kutumia penalti vizuri na kuondolewa," alisema Dabo.

Aidha, alisema kwa saa wanaenda kufanyia kazi kile alichokiona na kuhamisha nguvu zake kwenye michezo iliyopo mbele yao ikiwemo Ligi Kuu Tanzania Bara na kombe la FA.



Mchezaji wa mpira wa miguu wa Kituo cha Michezo cha Kili Youth Academy, King Mseke (wa pili kushoto), akiwania mpira na watoto wanaolelewa na Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete, wakati walipokuwa wakicheza mechi ya kirafiki katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Yanga sasa uso kwa uso na ...*

INATOKA UK. 24

Mshambuliaji mpya wa Yanga, Konkoni alikosa bao la wazi dakika ya 21 alipobaki yeye na kipa Innocent Mbonihankuye, lakini shuti lake lilitoka sentimeta chache nje ya lango.

Wadjibouti walikosa bao dakika ya 40 kupitia kwa beki wa zamani wa Simba Gilbert Kaze ambaye alikuwa nahodha katika mchezo huo.

Kaze anakumbukwa na mashabiki wa Simba aliposawazisha kwa kichwa bao la tatu dakika ya 84 katika mechi ya watani wa jadi ya Ligi Kuu iliyochezwa Oktoba 20, 2013 Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zikitoka sare ya mabao 3-3, Yanga ikitangulia kufunga mabao matatu kipindi cha kwanza na Simba kusawazisha yote kipindi cha pili.

Zouzoua aliyeingia kipindi cha pili alipachika bao la tatu dakika ya 54, alipowalamba chenga mabeki wa ASAS na kipa wao kabla ya kuujaza mpira wavuni.

Kipa Mbonihankuye aliumia katika purukushani hiyo, na akaingia Liban Said ambaye aliruhusu mabao mawili ya Mzize dakika ya 68 aliyeunganisha kwa kichwa krosi ya Nickson Kibabage, kabla ya Nzengeli kufunga bao la tano na la pili kwake katika dakika za nyongeza.

ASAS ilipata bao la kufutia machozi dakika ya 83 lililofungwa na Tito Mayor kwa mkwaju wa penalti baada ya yeye mwenyewe kuangushwa ndani ya eneo la hatari na mtokea benchi Zawadi Mauya.

## Simba kutumia mapumziko..

INATOKA UK. 24

"Nadhani maboresho ya muda huo yatasaidia kuwa na timu ya ndoto zetu wanasimba, tutarejea na nguvu na ubora zaidi," alisema Robertinho.

Aidha, alisema mara zote amekuwa akiwasisitiza wachezaji wake kuzingatia mazoezi na kuwa na nidhamu nayo ili kuwa imara zaidi na kuwa na timu ya ushindani kwa sababu anahitaji kupata ushindi kila mechi na kucheza mpira mzuri.

Robertinho alisema kipindi hiki ligi ikiwa imesimama atatumia pia kutengeneza muunganiko wa kila nafasi ikiwemo safu ya ulinzi ili kuwa imara na anapokosekana Che Fondoh Malone katika timu hiyo kuwe na mtu anayeweza kuziba nafasi yake.

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 27/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3815 | Oliveirense vs Penafiel | 2.34 | 3.22 | 2.81 |
| 13:15 | 2284 | PEC Zwolle vs Utrecht | 2.73 | 3.52 | 2.27 |
| 14:00 | 1642 | Rennes vs Le Havre | 1.46 | 4.54 | 7.02 |
| 14:00 | 3280 | Watford vs Blackburn | 1.99 | 3.42 | 3.37 |
| 14:30 | 2777 | St. Pauli vs Magdeburg | 1.85 | 3.75 | 3.65 |
| 14:30 | 3843 | Nurnberg vs Wehen | 2.00 | 3.55 | 3.35 |
| 14:30 | 4377 | Karlsruher SC vs Eintracht Braunschweig | 1.72 | 3.93 | 4.08 |
| 14:30 | 4514 | Arminia Bielefeld vs Jahn Regensburg | 2.13 | 3.53 | 3.06 |
| 15:00 | 1421 | Posta Rangers vs Bidco United | 2.19 | 2.89 | 3.35 |
| 15:00 | 2295 | Shabana FC vs Muranga Seal | 2.14 | 2.90 | 3.47 |
| 15:00 | 2324 | AFC Leopards vs FC Talanta | 1.63 | 3.21 | 5.71 |
| 15:00 | 2981 | Kolos Kovalivka vs Shakhtar Donetsk | 5.23 | 3.72 | 1.54 |
| 15:30 | 5506 | Feyenoord vs Almere City | 1.14 | 7.34 | 12.90 |
| 16:00 | 1063 | Strasbourg vs Toulouse | 2.17 | 3.56 | 3.25 |
| 16:00 | 1598 | Sheffield Utd vs Manchester City | 13.68 | 6.02 | 1.23 |
| 16:00 | 3730 | Burnley vs Aston Villa | 3.21 | 3.36 | 2.27 |
| 16:00 | 4426 | Montpellier vs Reims | 2.40 | 3.50 | 2.88 |
| 16:00 | 4456 | Clermont Foot vs Metz | 1.89 | 3.71 | 3.96 |
| 16:00 | 5934 | Santa Clara vs Vilaverdense FC | 1.58 | 3.63 | 5.31 |
| 16:30 | 5958 | Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.48 | 3.56 | 2.74 |
| 17:00 | 1226 | FC Liege vs Oostende | 2.44 | 3.36 | 2.57 |
| 17:00 | 3158 | St Truiden vs Cercle Brugge | 3.09 | 3.29 | 2.18 |
| 17:00 | 5048 | St Mirren vs Aberdeen | 2.22 | 3.23 | 3.08 |
| 17:00 | 5461 | Dundee FC vs Hearts | 2.88 | 3.32 | 2.29 |
| 17:30 | 2966 | Boavista vs Casa Pia Atletico | 2.21 | 3.14 | 3.19 |
| 17:45 | 4921 | Heerenveen vs Sparta Rotterdam | 2.24 | 3.47 | 2.82 |
| 18:00 | 2177 | Racing Ferrol vs Sporting Gijon | 2.29 | 2.92 | 3.21 |
| 18:05 | 2995 | Lorient vs Lille | 3.62 | 3.52 | 2.04 |
| 18:30 | 1265 | Bayern Munchen vs Augsburg | 1.14 | 8.56 | 17.97 |
| 18:30 | 1300 | Villarreal vs Barcelona | 3.39 | 3.49 | 2.14 |
| 18:30 | 2381 | Newcastle vs Liverpool | 2.17 | 3.86 | 3.03 |
| 18:30 | 5155 | Al Arabi Doha SC vs Umm-Salal SC | 1.53 | 3.98 | 4.84 |
| 19:00 | 2252 | Nordsjalland vs Midtjylland | 1.88 | 3.66 | 3.71 |
| 19:30 | 1461 | Fiorentina vs Lecce | 1.59 | 4.01 | 5.76 |
| 19:30 | 1488 | Juventus vs Bologna | 1.54 | 4.07 | 6.39 |
| 19:30 | 1873 | Al Sharjah SC vs Al Wasl Dubai | 2.01 | 3.43 | 3.13 |
| 19:30 | 2366 | Anderlecht vs Charleroi | 1.74 | 3.80 | 4.20 |
| 20:00 | 1766 | Vitoria Guimaraes vs FC Vizela | 1.86 | 3.33 | 4.07 |
| 20:00 | 3775 | AEL Limassol vs AEZ Zakakiou | 1.49 | 4.04 | 6.21 |
| 20:00 | 5414 | Sochi vs Lokomotiv Moscow | 2.34 | 3.45 | 2.68 |
| 20:15 | 3198 | Maccabi Tel Aviv vs FC Ashdod | 1.25 | 5.06 | 8.70 |
| 20:30 | 1104 | Mirandes vs Espanyol | 3.28 | 3.08 | 2.17 |
| 20:30 | 2266 | AL Wakrah vs Al-Shamal | 1.49 | 4.15 | 5.06 |
| 20:30 | 5426 | Valencia vs Osasuna | 1.94 | 3.44 | 4.11 |
| 21:00 | 1041 | PAOK vs Kifisias | 1.22 | 5.44 | 13.59 |
| 21:45 | 2034 | Napoli vs Sassuolo | 1.39 | 5.14 | 7.23 |
| 21:45 | 3219 | Nice vs Lyon | 2.14 | 3.64 | 3.23 |
| 21:45 | 4413 | Lazio vs Genoa | 1.58 | 4.00 | 5.96 |
| 22:30 | 5514 | Athletic Bilbao vs Betis | 1.92 | 3.61 | 3.97 |
| 22:30 | 5782 | Sporting Lisbon vs Famalicao | 1.23 | 5.80 | 10.00 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Agosti 27, 2023
Nipashe



UK. 22

## Lukaku kupelekwa Roma kwa mkopo

# YANGA SASA USO KWA USO NA AL MERREIKH

### ●●● Ni katika raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika...

**Na Adam Fungamwango**

NI rasmi sasa Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga, watacheza mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merreikh ya Sudan.

**Hatua hiyo ni baada ya kuinyoa Asas FC ya Dji bouti kwa mabao 5-1 katika mchezo wa marudiano hatua ya awali ya michuano hiyo iliyofanyika jana Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.**

Katika mechi hiyo ya hatua ya awali, Yanga imesonga mbele kwa jumla la mabao 7-1 kutokana na Jumapili iliyopita kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa pia kwenye uwanja huo kufuatia Asas FC kuomba kuutumia kama uwanja wake wa nyumbani.

Yanga itacheza na Al Merreikh kutafuta tiketi ya kuingia hatua ya makundi ya michuano hiyo na mchezo wa kwanza utachezwa Septemba 15 Yanga ikianzia ugenini na kurudiana Dar es Salaam Septemba 29.

Al Merreikh imeingia hatua hiyo baada kuitoa Otoho d'Oyo ya Congo Brazaville ikilazimisha sare ya bao 1-1 ugenini na kusuluhu juzi kwenye Uwanja wa Huye, Butare nchini Rwanda ambako inatumia kama uwanja wa nyumbani kutokana na machafuko nchini Sudan, hivyo imefuzu kwa bao la ugenini.

Yanga imepata ushindi mwingine wa mabao matano siku chache tu baada ya Jumatano iliyopita kuisulubu KMC mabao 5-0, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa katika uwanja huo huo.

Walikuwa wachezaji wapya waliosajiliwa msimu huu, Maxi Nzengeli aliyefunga mabao mawili, Hafiz Konkoni, Pacome Zouzoua, na moja la mchezaji mzawa aliyetokea benchi kwenye mchezo wa jana Clement Mzize waliopeleka kilio cha mabao hayo.

Yanga ilianza mechi kwa kasi na iliwachukua dakika moja kufanya shambulizi la nguvu kwenye lango la wapinzani wao, pale Jesus Moloko alipoondoka na mpira kwenye wingi la kulia na kupiga krosi iliyounganishwa kwa mguu wa kushoto na Stephane Aziz Ki lakini ukatoka pembeni kidogo ya lango.

Asas ilijibu shambulio hilo dakika ya tano baadae pale krosi ya Youssouf Abdi Ahmed wingi ya kulia ilipounganishwa kwa kichwa na Abbas Abdourahman, lakini mpira ukapaa juu ya lango la Yanga.

Yanga ilipata bao la kwanza dakika ya saba likifungwa na Maxi Zengeli , akiunganisha kwa kichwa krosi kutoka kwa Moloko.

Bao hilo lilitokana na wachezaji wa ASAS kujichanganya wenyewe kuokoa mpira ambao uliwakuta wachezaji wa Yanga walioupora na kutengeneza shambulizi hilo.

Dakika tatu baadae Aziz Ki alikaribia kuipa Yanga bao la pili lakini shuti lake la kushtukiza lilipaa juu kidogo ya lango la Asas FC.

Baada ya hapo ni kama Yanga iliridhika na kupunguza kidogo mashambulizi, huku wageni wao wakionekana kutulia na kucheza pasi fupi fupi ambazo hata hivyo hazikuwa na msaada mkubwa kwao wala madhara kwa wenyeji wao.



Kiungo wa Yanga, Max Nzengeli (kulia) akimpongeza mchezaji mwenzake, Pacome Zouzoua baada ya kuifungia timu hiyo bao la nne dhidi ya Asas FC katika mchezo wa marudiano wa hatua ya awali ya klabu bingwa Afrika jana kwenye Uwanja wa Azam Complex Dar es Salaam, Yanga ilishinda mabao 5-1 na kusonga mbele hatua inayofuata kwa jumla ya mabao 7-1. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

INAENDELEA UK. 23

## Simba kutumia mapumziko kusaka makali zaidi

**Na Saada Akida**

KOCHA mkuu wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho' amesema atatumia siku 16 za mapumziko kukiimarisha zaidi kikosi chake na kuongeza makali kwenye idara.

Alisema siku hizo 16 kwake atazitumia kikamirifu kuhakikisha wanarejea uwanjani wakiwa na makalimara mbili zaidi ya sasa.

Robertinho ametoa kauli hiyo huku Simba ikiwa inaongoza ligi kwa kuwa na pointi sita baada ya kucheza michezo miliwi ya Ligi Kuu Bara msimu huu huku wakiwa wamefunga jumla ya mabao sita na kuruhusu mabao mawili.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema kwa kuwa wanaenda kwenye mapumziko mafupi ya Ligi Kuu kwa ajili ya kupisha michezo ya timu za Taifa, amepanga kuendelea na programu zake za mazoezi.

Alisema anahitaji muda mwingi wa kuendelea kukisuka kikosi cha timu yake hiyo huku kundi la pili ambalo lilichelewa kujiunga kwenye 'Pre Season' wanaenda sawa na kundi la kwanza lililowai kwenye maandalizi yao Uturuki.

"Nimetoa mapumziko kwa wachezaji ambayo yatachukua siku nne na kurejea kikosini, baada ya hapo tutatumia siku 16 kujiandaa, unajua wakati wa maandalizi yetu Uturuki kuna wachezaji walichelewa kufika sasa tutatumia siku hizi kuweka mambo sawa na kuongeza makali yetu kwenye nafasi zote," alisema Robertinho.

Alisema baada ya siku hizo kikosi chake kitarejea kwenye michezo yake ya ligi kuu kwa kasi na nguvu zaidi.

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042